epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumanne Desemba 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581886

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital 0677 020 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ LIKE & FOLLOW US

RIPOTI MAALUMU **DAWA ZA KULEVYA:**

# Mbinu mpya za wauzaji ni balaa

• **Mitandao** ya siri yatumika, dawa mpya 1,184 zaingizwa sokoni; madaktari bingwa, wachumi watoa angalizo... *Ukurasa 2*

UKURASA WA 3

**Gwajima** asema ukatili wa kijinsia umepungua

UKURASA WA 4

**Makonda** aituliza BAKWATA hoja kupatiwa eneo la wazi Arusha

UKURASA WA 19

**Naibu** Rais Kenya amjibu Gachagua kuchelewa kuunda Tume ya Uchaguzi

## Pacha walioungana watenganishwa, kukaa Muhimbili mwaka mmoja

UKURASA 3



Hadija Shaban akisukuma kiti kilichobeba watoto wake mapacha, Hassan na Hussein (3), alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam jana baada ya kurudi kutoka Saudi Arabia. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**



## Rais Samia asamehe wafungwa 1,548, wamo pia waliohukumiwa kunyongwa

UKURASA 3

**MICHEZO** FADLU AANIKA SABABU KIPIGO SIMBA ALGERIA UK.24 **MAONI,** UK.6

RIPOTI MAALUMU

# Mbinu mpya wauzaji dawa kulevya balaa

Na Maulid Mmbaga



Wauzaji dawa za kulevya hivi sasa wanatumia mitandao ya siri kuuza bidhaa

WAUZAJI dawa za kulevya wamebadili mbinu, wakiibuka na njia mpya, zikiwamo za medani za kivita, ili kukwepa kukamatwa, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imethibitisha.

Kwa mujibu wa mamlaka hiyo, hivi sasa wauzaji wa dawa hizo pamoja na mbinu zingine, wanawasiliana kwa mitandao ya siri (dark webs), wanasafirisha dawa kwa ndege nyuki (drones), vipuri vya magari, nguo za asili, vinyago, simu na vikapu.

Vilevile, imebainika wauzaji wa dawa hizo wana boti maalumu za usafirishaji wa dawa ambazo zina mwendo mkali kulinganishwa na boti za mamlaka za udhibiti, hivyo kutowakamata kirahisi.

Kamishna wa DCEA, Peter Patric amemwambia mwandishi wa habari hii kuwa wamebaini mbinu hizo baada ya mamlaka hiyo na Jeshi la Polisi kuweka mikakati ya kukomesha matumizi na usambazaji wa dawa hizo nchini.

Anasema kuwa mbali na kubadili mbinu za usafirishaji, wauzaji dawa za kulevya sasa wanaingiza sokoni aina mpya za dawa ambazo haziko kwenye majedwali ya wadhibiti. Anabainisha kuwa kuna dawa mpya 1,184.

"Kwa msingi huo, mataifa mbalimbali, ikiwamo Tanzania, yameanza kuziongezea uwezo maabara za sayansi jinai pamoja na maofisa wanaohusika na vitengo hivyo ili wawe na uelewa wa utambuzi wa aina hizo mpya za dawa ambazo zinaingizwa sokoni kinyume cha sheria.

"Hivi sasa dawa za kulevya si tu zinasafirishwa kwa ndege, boti na meli kama zamani, bali pia zinauzwa katika mataifa mbalimbali kupitia dark webs (mitandao ya kijicho/siri).

"Kupitia mitandao hiyo, mtu anaweza kusema 'mimi ninataka kete tano za Heroin', kisha akatuma fedha kwa njia ya mtandao na dawa hizo zikasafirishwa kama bidhaa nyingine kumfikia aliyeagiza. Kwa hiyo, mtu anapokea mzigo, ukiangalia unadhani ni simu, kumbe ni dawa za kulevya," anafafanua.

Kamishna Patric anasema wamekamata kiwango kikubwa cha dawa zinazotoka nchini kwenda nje kwa kutumia vifaa kama vile vipuri vya magari, vyuma, vikapu na nguo za kiasili.

Anaeleza kuwa katika uwanja wao huo, upelelezi wa aina hiyo ya uhalifu ni mgumu na unahitaji vyanzo vingi na ushirikiano mkubwa na mataifa mengine kujua dawa husika imetoka wapi ili kuhakikisha unaidhibiti.

Kuhusu aina mpya za dawa za kulevya, Kamishna Patric anabainisha kuwa kati ya dawa hizo, zimo zinazoitwa "New Psychotropic Substances - NPS", akiwa na ufafanuzi kwamba awali zilikuwa zinalimwa shambani mithili ya bangi, lakini hivi sasa zinatengenezwa viwandani na zinakuwa na ladha sawa na zilizokuwa zinalimwa shambani.

"Ripoti ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2023, inaonesha kulikuwa na aina mpya ya dawa hizo 1,184 zilizoingia katika soko la dunia," anasema.

Kamishna Patric ana lingine la ziada; wamebaini meli zinazotumika kusafirisha dawa hizo zinapokuwa katikati ya maji ya kimataifa, boti za wahalifu hutoka nchi kavu na kuzifuata huko kuchukua dawa.

Anaeleza sifa za boti hizo kwamba zina uwezo mkubwa wa kukimbia kushinda boti za wakaguzi, hali inayowawia ugumu kuwakamata wahalifu hao. Wanahitaji vifaa vya kisasa na wataalamu wenye uwezo mkubwa kukabiliana na uhalifu huo.

### MATUMIZI YA DAWA

Kamishna Patric anasema dawa za kulevya zinazotumika zaidi nchini ni bangi, mirungi, Heroin, Cocaine na tiba zenye asili ya kulevya ambazo zinatumika pia hospitalini.

Anasema asilimia 85 ya Heroin inayotumika duniani kote inatoka Afghanistan. Matarajio yao kiwango cha uingizaji dawa hizo nchini kitashuka kutokana na kundi la Talbani kuchukua madaraka. Kundi hilo limepiga marufuku kilimo cha 'Pop Plant', zao linalozalisha Heroin.

"Hii dawa huletwa nchi za mashariki na kusini mwa Afrika kuanzia Somalia, Kenya (hasa Mombasa), Tanzania (hasa Tanga, Mtwara na Lindi), Msumbiji mpaka Afrika Kusini (hasa Cape Town) kupitia Bahari ya Hindi kwa sababu zikizalishwa Afghanistan zinakwenda Iran au Pakistani.

"Utafiti unaonesha kwamba, kati ya tani 50 na 100 za dawa za kulevya aina ya Heroin zinapita katika ukanda huu wa mashariki na Afrika, lakini kiasi kinachotumika nchini ni chini ya tani 10.

"Hali hii haina maana kwamba sisi ni wazembe wa kudhibiti, hapana! Ni kutokana na uhalisia wa jiografia ya nchi yetu. Hivyo, iwe jua au mwezi, ni lazima wapitishe hapa ili kwenda Ulaya, China, Marekani na Australia," anasema Kamishna Patric.

Anabainisha kuwa ripoti za matumizi ya dawa za kulevya zinaonesha mwaka 2022 kulikuwa na watu milioni 292 duniani wanaotumia dawa hizo. Kati yao, milioni 228 wanatumia bangi na milioni 13.9 wanatumia dawa zingine kwa njia ya kujidunga.

Kamishna Patric anafafanua zaidi kuwa kati ya watu milioni 13.9 wanaojidunga dawa hizo, milioni 6.8 wanaishi na virusi vya homa ya ini na milioni 1.6 wanaishi na Virusi vya Ukimwi (VVU).

"Kwa Tanzania utafiti uliofanyika mwaka 2014, unaonesha kulikuwa na watu 250,000 hadi 500,000 waliokuwa wanatumia dawa za kulevya aina ya Heroin. Kati yao, 30,000 walikuwa wanatumia kwa njia ya kujidunga.

"Wakati huo, watu wengi waliokuwa wanatumia dawa hizo walikuwa wanaishi Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma ambayo hivi sasa inakuja juu kwa kuwa na idadi kubwa. Utafiti unaonesha asilimia 36 ya watu wanaotumia dawa kwa njia ya kujidunga, wanaishi na VVU.

"Hali ni mbaya zaidi kwa wanawake. Utafiti unaonesha kuwa, kati ya wanawake 100 wanaojidunga nchini, 60 walikuwa wanaishi na VVU. Pia asilimia 90 ya kundi hilo wanafanya biashara ya ngono ili kupata fedha ya kununulia dawa hizo," Kamishna Patric anafafanua.

### MADHARA KIAFYA

Dk. Saidi Kuganda, Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Idara ya Afya na Magonjwa ya Akili, anasema dawa za kulevya zina madhara mengi kiafya ya mwili kulingana na aina ya dawa, kiwango cha matumizi na muda wa matumizi. Pia zina madhara kwa akili na kijamii.

Dk. Kuganda ambaye pia Mwenyekiti wa Chama cha Wataalam wa Afya ya Akili Tanzania (MEHATA), anayataja madhara kwa mwili, akisema:

"Yanajumuisha magonjwa ya mfumo wa upumuaji; kuvuta dawa kama bangi au Cocaine husababisha matatizo ya mapafu, saratani ya mapafu na magonjwa ya upumuaji kama pumu.

"Pia kupata magonjwa ya ini. Matumizi ya dawa kama heroin yanaweza kusababisha ugonjwa wa ini (cirrhosis) na kushindwa kufanya kazi kwa ini.

"Magonjwa ya moyo; dawa kama Cocaine na Methamphetamine husababisha shinikizo la damu, mapigo ya moyo kutokuwa ya kawaida, na hatari ya mshtuko wa moyo.

"Matumizi ya sindano zisizo safi husababisha maambukizi ya magonjwa kama vile HIV na hepatitis (homa ya ini). Pia kupunguza uzito kupita kiasi kwa sababu dawa nyingi hupunguza hamu ya kula na kusababisha utapiamlo.

"Madhara mengine ni magonjwa ya ngozi na kinywa, dawa za kulevya kama Heroin husababisha hitilafu katika mfumo wa umeme wa ubongo na kuleta kifafa ikiwa itatumika nyingi kupita kiasi au wakati wa kujaribu kupunguza au kuacha ghafla."

### MADHARA KIUCHUMI

Mhadhiri na Mtaalamu wa Biashara na Uchumi katika Chuo cha Biashara (CBE), Dk. Mariam Tambwe, anasema matumizi ya dawa za kulevya yana madhara makubwa kiuchumi kwa kuwa waraibu wakishatumia dawa, hawawazi kwenda kufanya kazi badala yake wanafikiria kwenda kuiba na kupora.

Anasema wengi wao wakishatumia dawa, wanakuwa wanasinzia na kutokujihusisha na shughuli za uzalishaji, huku wengine wakifikia hatua ya hata kwenda kuiba majumbani mwao ili kupata fedha ya kununulia dawa hizo, jambo ambalo linachangia kurudisha nyuma uchumi wa familia.

"Ushauri wangu kwa mamlaka husika, waongeze kasi katika kuzuia uingizwaji dawa za kulevya nchini, viongozi wa dini wasaidie kuwapa elimu ya kiimani vijana na watanzania kwa ujumla juu ili wajiepushe na matumizi ya dawa hizo.

"Vilevile, wale vijana wote waliothirika kutokana na matumizi ya dawa hizo, wapewe usaidizi wa matibabu hospitalini, wakishapona wawezeshwe mitaji ya kufanya shughuli za kimaendeleo, pia wakasaidie kutoa elimu kwenye jamii juu ya madhara ya dawa hizo na kujiepusha nazo," anasema Dk. Mariamu.

### MIKAKATI MINNE

Katika kukabiliana na madhara hayo, Kamishna Patric anasema wanayo mikakati mikuu minne, ukiwano wa kuhakikisha wanapunguza uingizaji, uzalishaji na usambazaji dawa za kulevya nchini.

Anataja mkakati wa pili ni kupunguza mahitaji kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yake ili watu wasijiingize katika matumizi ya dawa hizo na kuwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

Kamishna Patric anataja mkakati wao wa tatu ni kupunguza madhara yanayotokana na dawa za kulevya kwa kusimamia na kutoa ushauri kwa watumiaji kuhakikisha wanatumia dawa sahihi ili wasipate madhara.

"Kwenye kupunguza madhara tunatibu na kusimamia matibabu ya waraibu wa dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali kama nyumba za matibabu kwa waraibu na hospitalini ili kuhakikisha kwamba waathirika wanapata matibabu," anasema.

Anataja mkakati wao wa nne ni kuimarisha ushirikiano wa kitaifa na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na udhibiti wa dawa za kulevya kikanda na kimataifa kwa lengo kuhakikisha wanawadhibiti wauzaji wa dawa hizo ambao hawana mipaka.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Wataalamu wanaonya kuwa matumizi ya dawa za kulevya yana madhara kiafya, kiuchumi na kijamii

HABARI KITAIFA

# Samia asamehe wafungwa 1,548, wamo waliohukumiwa kunyongwa

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa msamaha kwa wafungwa 15,48 kati yao 22 wameachiwa huru jana na 1,526 wamebaki gerezani kumalizia sehemu ya kifungo kilichobaki.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeeleza kwamba msamaha huo sehemu ya kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

"Rais Samia ametumia mamlaka aliyopewa chini ya Ibara ya 45(1)(a)-(d) ya Katiba ya Jamhuri kutoa msamaha kwa wafungwa kwa masharti mbalimbali."

"Ni matarajio ya serikali kuwa wafungwa walioachiwa huru leo (jana), watarejea tena katika jamii kushirikiana na wananchi wenzao katika ujenzi wa taifa letu na watajiepusha kutenda makosa ili wasirejee tena gerezani."

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, wafungwa waliopata msamaha huo ni waliohukumiwa adhabu ya kuanzia miaka miwili na kuendelea ambao wametumikia robo ya adhabu zao gerezani na walioingia kabla ya Oktoba 19, mwaka huu.

Alisema wafungwa wote waliotumikia kifungo cha maisha gerezani bila kujali kosa, ambao wametumikia adhabu zao kwa miaka 15 na kuendelea, wamebadilishiwa adhabu zao kuwa kifungo cha miaka 30 kuanzia tarehe ya hukumu.

Pia wafungwa waliobadilishiwa adhabu kutoka adhabu ya kifo na kuwa cha maisha ni kwa waliotimiza miaka 10 kuendelea tangu kupata msamaha huo, sasa watatumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

Wengine ni wenye magonjwa ya kudumu au sugu ambao wapo kwenye hatua ya mwisho na imethibitishwa na jopo la waganga, wafungwa wazee wenye umri wa miaka 70 na zaidi, wajawazito waliofungwa gerezani.

Pia, wapo wafungwa wanaokabiliwa na ulemavu mkubwa wa mwili au akili unaozuia uwezo wao wa kufanya kazi, wafungwa ambao hukumu zao za kifo zimebadilishwa na kuwa kifungo cha maisha, wafungwa ambao wametumikia angalau miaka 15 bila kujali aina ya uhalifu, na wale waliokamatwa na kushikiliwa kwa zaidi ya miaka 10.



Wengine ni wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 10 au zaidi.

Aidha, msamaha huo hautahusisha wafungwa wanaotumikia vifungo vya nje na wale waliowahi kukiuka masharti ya Sheria ya Parole na kurudishwa gerezani kutumikia adhabu zao.

Pia, wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani ambacho sio cha maisha kwa makosa ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, rushwa na usafirishaji au kujihusisha kwa namna yoyote na madawa ya kulevya ikiwamo bangi.

Wengine ni waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani ambacho sio cha maisha kwa makosa ya kujamiiana, utekaji, au wizi wa watoto, kupoka, kuwapa mimba wanafunzi au makosa yoyote yanayohusiana na ukatili dhidi ya watoto na kujihusisha kwa namna yoyote ile na biashara haramu ya binadamu.

Aidha, wengine ni wafungwa waliopatikana na hatia ya kuhukumiwa kifungo gerezani ambacho sio cha maisha kwa makosa ya kukutwa na viungo vya binadamu, unyang'anyi wa kutumia nguvu, kutumia silaha, kumiliki silaha, risasi, milipuko au kujaribu kutenda makosa hayo.

Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani ambacho sio cha maisha kwa makosa ya kujihusisha kwa namna yoyote na nyara za serikali, au ujangili.

Wanaotumikia kifungo kisicho cha maisha kwa makosa ya wizi au ubadhilifu wa fedha za serikali, waliohukumiwa adhabu ya kifo, kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutendeka kwa makosa hayo.

Wenye makosa ya kujaribu kuua, kujiua au kuua watoto wachanga, ugaidi, uharamia na makosa ya kimtandao.

Wanaotumikia kifungo cha pili au warudiaji na wale waliowahi kupata msamaha wa raia, na waliotenda makosa ya kinidhamu gerezani ambayo makosa yao hayajatimiza miaka mitatu hadi Desemba 9, mwaka huu, na wafungwa wa madeni.

Katika kurasa za mtandao wa kijamii, Rais Samia Suluhu Hassan, aliandika ujumbe katika kuadhimisha miaka hiyo ya Uhuru kwa kuwataka Watanzania kutumia siku hiyo kumshukuru Mungu kwa hatua kubwa ambayo nchi inaendelea kupiga.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Waziri Gwajima asema ukatili wa kijinsia umepungua nchini

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima amesema ukatili wa kijinsia umepunguza kwa kiwango kikubwa nchini, huku takwimu za mwaka 2022 zikionesha mikoa ya Manyara na Arusha inaongoza kwa kadhia hiyo kwa asilimia 43.

Dk. Gwajima alibainisha hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Mapambano dhidi ya Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika Nyamongo, wilayani Tarime, mkoa wa Mara.

Alitaja mikoa inayofuatia kwa kupunguza ukatili huo kuwa ni pamoja na Mara asilimia 28, Singida asilimia 20, Tanga asilimia 19 na Dodoma asilimia 18.

"Kama Mara wameweza kupunguza ukatili wa kijinsia, wewe umekwama wapi sasa? Ifike mahala ukatili ufike mwisho, maana ukeketaji umepungua kwa asilimia mbili, mkiendelea kupunguza ukatili hadi asilimia 10 ninawaahidi wazee wa mila mtapanda ndege kwenda kutembea Ulaya," alisema Dk. Gwajima.

Alisema lengo ni kuhakikisha ukatili unadhibitiwa kabisa nchini kwa kushirikisha jamii kupitia elimu, hususani katika maeneo ya vijijini, shule za msingi na sekondari, vikundi, mashirika, wazee wa kimila pamoja na viongozi wa dini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime/Rorya, Marck Njera alisema ukatili wa kijinsia katika eneo hilo umepungua kwa kiwango kikubwa kulinganisha na miaka ya nyuma. Lakini ana taarifa koo 13 za kabila la Wakurya wamejiandaa kwa ukeketaji mwezi huu.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi Tanzania, Naibu Kamishna (DCP) Mary Nzuki, alisema kwa kipindi cha siku 16 kuanzia Novemba 25, jeshi hilo lilipeleka askari polisi 250 kutoka mikoa mbalimbali nchini na kufanikiwa kutoa elimu katika shule za msingi 26, makanisa 43, misikiti 20 huku wakiwafikia wanafunzi 130,000, wananchi 96,000, vikiwamo vikundi vya vijana, wazee na ngariba.

***Imeandaliwa na Timoth Itembe na Samson Chacha (TARIME)**

# Pacha walioungana watenganishwa, kukaa Muhimbili mwaka mmoja

**Na Christina Mwakangale**

WATOTO mapacha Hussein na Hassan Jumanne (3), waliokuwa wameungana baadhi ya viungo vya mwili, ikiwamo kibofu cha mkojo na utumbo, wamerejea nchini wakitokea Saudi Arabia, walikokaa kwa mwaka mmoja na miezi minne kwa ajili ya kutenganishwa.

Hussein na Hassan, waliondoka nchini Agosti 23, mwaka jana, kwenda kufanyiwa upasuaji Oktoba 5, mwaka jana, na iliwachukua madaktari saa 16 kuwatenganisha katika hospitali ya King Abdulaziz, iliyoko Riyadh, Saudi Arabia.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Rachel Mhavile, akizungumza jana, jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), alisema kutokana na watoto hao kuzaliwa wakiwa viungo vimeungana sehemu tatanishi, ililazimika kupelekwa nchini huko.

"Tumekuja kuwapokea watoto, pamoja na mama yao waliokaa Saudi Arabia kwa takribani mwaka mmoja, kabla walikaa MNH mwaka mmoja na zaidi wakisubiri kukua na kuwa katika hali nzuri kwa ajili ya kwenda kwa wenzetu kusaidia matibabu," alisema Dk. Mhavile.

Alieleza kuwa awali, Hadija alipojifungua alipatiwa huduma zote MNH, lakini ilipofika suala la kuwatenganisha wadau wengine walihitajika. "Haya ni matibabu ya awamu ya kwanza ya kuwatenganisha, sasa tunarudi nao MNH tunawapa nyumba ya kuishi mojawapo kwa mwaka mzima tena na baada ya mwaka watarudi tena Saudi Arabia.

"Upasuaji wa hawa watoto walioungana huwa inategemeana wameungana sehemu zipi, wakiwa wameungana maeneo ambayo ni 'complex' au tata kama moyo, uti wa mgongo, sehemu za siri au wanajumuika miguu.

"Kwa mfano, hawa walikuwa na miguu mitatu. Kila mmoja ana mguu imara ila ule wa tatu haujaimarika, ilihitaji ubingwa zaidi ambao sisi bado tunauhitaji, Saudi Arabia, imekubali kutusaidia, lakini bado na kwetu wanajifunza," alisema Dk. Mhavile.

Dk. Mhavile ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji MNH, alisema pia mapacha hao watakaporejea Saudi Arabia watapatiwa mguu wa pili wa bandia kila mmoja, baada ya mguu wa tatu kuondolewa ambao ulikuwa dhaifu.

Bingwa wa Upasuaji wa Watoto MNH, Dk. Zaitun Bokhary, alisema upasuaji wa watoto hao ulifanyika jijini Riyadh, Oktoba 5, mwaka 2023 kwa saa zipatazo 16 ukiwashirikisha wataalamu mbalimbali wakiwamo mabingwa wa watoto, mifupa, kibofu cha mkojo na mishipa ya fahamu na damu.

"Watoto hawa waliungana kuanzia kifua, tumbo, nyonga, waliungana kwa ndani utumbo mkubwa na baadhi ya mishipa ya damu iliungana na eneo lililokuwa tatanishi zaidi ni kibofu cha mkojo. Mmoja kilikuwa wazi kwa nje, mwingine kilikuwa kimefunika wa ndani, ni eneo tata, lilolihitaji kuhusisha mabingwa wa kibofu cha mkojo wasiopungua wanane.

Pia, madaktari bingwa wa mifupa walihitajika kuutenganisha mguu wa tatu na kuuondoa, sasa wote wana mguu mmoja mmoja, kituo walikofanyiwa upasuaji wana uzoefu wa upasuaji wa aina hii na wamebobea kwa miaka zaidi ya 30," alisema D. Zaitun.

Hadija Shaban (24), mama wa watoto hao aliishukuru serikali pamoja na Saudi Arabia, kwa kuwa akiwa nchini humo iliwagharamia kuanzia matibabu pamoja na huduma zote za mlo na malazi.

"Mimi ndio baba, ndio mama, MNH ndio ndugu zangu, wa kwangu hawajwahi kutokea hata siku moja, na Dk. Zaitun, ni mama yangu, Mungu amzidishie. Nilipotoka Igunga, Tabora hadi kwenda Saudi Arabia, alinisaidia hata katika kuwasiliana nikiwa huko kwa sababu binafsi sijui lugha ya Kiarabu wala Kiingereza," alisema Hadija.

Kadhalika, Hadija aliomba msaada wa kupatiwa uwezeshaji wa makazi kwa kuwa atahitajika kukaa mkoani Dar es Salaam, wakati akiendelea na matibabu kwa zaidi ya mwaka mmoja.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Makonda aituliza BAKWATA hoja kupatiwa eneo la wazi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda amemtaka Shekhe wa Mkoa huo, Shaaban Bin Jumaa kuwa na subira na ombi lake alilotoa kwa Rais Samia Suluhu Hassan la kupatiwa eneo la wazi la mnara wa Mwenge.

Amesema wanapaswa kuwa wavumilivu kwa kuwa suala hilo liko katika hatua za mwisho ili wakabidhiwe hati ya eneo hilo.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akihitimisha matembezi ya kuombea amani mkoa wa Arusha na taifa ikiwa ni maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Makonda alionya kuwa asiwapo mtu yeyote akawapa hofu juu ya eneo hilo.

"Shekhe wetu alimwomba Rais apewe eneo hili, ili waendeleze imani yao na akaniambia kuna jambo limekwama, ila leo (jana) ninapenda kusema Rais Samia alichoahidi kwa shekhe wetu kitatimia, asiwapo mtu akawapa hofu, taratibu zinaendelea.

"Na tayari nimemwona Waziri wa Ardhi, naye amenihakikishia anakamilisha mchakato na timu yake na atakapokamilisha tutakuja kukukabidhi hati. Maelekezo ya Rais wetu ni sheria. Ninaomba tuwe wavumilivu," alisema.

Makonda alisema kila mmoja anapaswa kurudi kwenye magoti ya Mungu, ili kila mmoja awe na maendeleo na kuepukana na mikosi na balaa.

"Ebu tuwe na muda wa kuomba na kila mmoja anapewa muda mwenyewe unatabiri mema katika maisha yako, ili adui anapotafuta hatia, yale maneno yanasimama katika maisha yako, halafu wewe kimbia maombi...

"Mimi sina uadui na mtu licha ya kuwa kuna wakati sikuwa na kazi miaka mitatu na miezi sita, niliishi bila mshahara na nikawajua watu, ila nimeweka agano kwa Mungu wangu tangu nilipopata uenezi mshahara wote niliweka madhabahuni mwa Mungu, hivyo ukichezea kiti unachezea kiti cha Mungu mwenyewe, utakutana na Mungu mwenyewe anayepokea mshahara wake," alisema na kuibua kicheko.

Makonda pia alisema mkesha wa mwaka mpya 2025 utafanyika kwenye mzunguko wa mnara wa Saa, jijini Arusha na nchi 12 zitashiriki kwa kula nyama na kunywa na ikitimu saa 5:40 usiku, watumishi wa Mungu watasimama kuongoza maombi hadi saa 6:00 usiku.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Mariadhiano na Amani Tanzania (JMAT), Dk. Israel Ole Maasa alisema Makonda amechagua fungu jema, nalo halitaondolewa.

Shekhe wa Mkoa wa Arusha, Shaaban Bin Jumaa aliombea nchi dhidi ya maadui wa ndani na nje ya nchi, ili vizazi vilivyopo na vijavyo viendelee kunufaika na amani iliyopo.

Laigwanani Mkuu wa Jamii Wamasai Tanzania, Isack Ole Meijo alimwombea Rais Samia na viongozi wote wa serikali afya njema.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Abiria wa boda-boda akiwa amekaa nyuma ya mzigo wake bila kujali usalama wake, kama alivyonaswa na kamera yetu eneo la Kifuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TCRA yajivunia kushuka gharama mawasiliano miaka 63 ya Uhuru

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema kuwa gharama za simu zilishuka kwa asilimia 946 kati ya mwaka 2005 na Septemba mwaka huu.

Aidha, gharama zimeshuka kutoka Sh. 219 kwa dakika mwaka 2005 hadi Sh. 26, Juni 2024 kwenye mtandao wa mtumiaji na kutoka Sh. 292 kwa dakika hadi Sh. 28 mitandao mingine Septemba 2024.

Taarifa iliyotolewa kwa umma na TCRA katika maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru, ilieleza fursa zilizopo kwenye mawasiliano ambazo zimewezesha wananchi kuendesha maisha yao kwa ufanisi kupitia huduma na teknolojia mpya.

Pia, TCRA imesema wananchi wana uhuru zaidi wa kuchagua huduma na kukamilisha miamala kwa gharama nafuu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari alisema kushuka kwa gharama kati ya mitandao kumewapa watumiaji uhuru wa kupiga simu kwenye mitandao mingine bila kulazimika kuwa na laini za mitandao hiyo.

"Takwimu zinaonesha kuwa kati ya 2019 na 2023 kiwango cha ukuaji wa muda wa maongezi kwenda mitandao mingine kilikuwa mara saba ya kile cha muda ndani ya mtandao wa mtumiaji," alisema.

Aidha, alisema kushuka huko kumechangiwa na gharama za kuunganisha simu kati ya mitandao kwa dakika, kutoka Sh. 15.6 mwaka 2018 mpaka Sh.1.76 Januari 2024.

"Kukua kwa huduma za simu za mkononi kumewezesha kukua kwa huduma tegemezi, ambazo zimewapa wananchi uhuru zaidi wa kuwasiliana na kufanya miamala mbalimbali," alisema.

Dk. Bakari alifafanua kuwa kukua kwa akaunti za pesa kwa simu za mkononi, ambazo zimeongezeka kwa asilimia 245 kati ya 2015 na Septemba 2024, na kwamba zilifikia 60,815,533 Septemba, mwaka huu kutoka 17,639,349.

"Huduma za fedha kupitia simu za mkononi zimeleta ufanisi kwa watumiaji na pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi," alisema.

Vilevile, alisema malipo ya kielektroniki yanawezesha mamlaka zinazosimamia mapato kudhibiti mapato ya serikali na sekta ya umma.

"Septemba 2024 kulikuwa na laini za simu 80,662,041 ikilinganishwa na 110,518 mwaka 2000. Kulikuwa na laini 79,646,221 za mawasiliano kati ya watu na 1,015,820 zinazotumika kwa mawasiliano ya mashine zenyewe bila kuingiliwa na binadamu," alisema.

Aidha, alisema kuongezeka kwa laini za mashine kunaashiria kuenea Tanzania kwa teknolojia za kidijiti zinazojiendesha zenyewe, laini za aina hii zilikuwa 962,928 Juni 2024.

"Simu za mezani zimeongezeka kutoka 16,238 mwaka 1961, ambapo 7,421 au asilimia 54.3 zilikuwa Dar es Salaam pekee, hadi 78,048 Septemba 2024," alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, ujio wa simu za mkononi na teknolojia mpya umeathiri kuongezeka kwa simu za mezani kwani simu za aina hii zilikuwa 275,591 mwaka 2000.

Aidha, alisema watumiaji wa intaneti waliongezeka kwa asilimia 1,061 kutoka 3,563,732 mwaka 2008 hadi 41,376,545 Septemba 2024.

# NBS, REA kufanya utafiti wa nishati ya kupikia Tanzania Bara

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) zinatarajia kuanza utafiti wa tatu kuangalia hali ya upatikanaji nishati kwa Tanzania Bara mwaka 2024.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema hayo mjini hapa wakati akizungumza na wadadisi 110 waliokuwa wanafundishwa namna ya kufanya utafiti huo kutoka kwa wataalamu mbalimbali wakiwamo wa kutoka Wizara ya Nishati, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na NBS.

Dk. Chuwa alisema utafiti huo utazifikia kaya 10,500 za Tanzania Bara za mijini na vijijini pamoja na kuangalia matumizi ya nishati ya kupikia.

"Utafiti huu ni muhimu sana katika kutekeleza Maendeleo Endelevu ya Dunia ya mwaka 2030, Dira ya Taifa ya 2025 inayomalizika na ambayo haiwezi kumalizika bila kuwa na taarifa sahihi na ile ya 2025 hadi 2050, " alisema.

Dk. Chuwa alisema kuwa katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, hali ya wananchi kutumia nishati safi ilikuwa ndogo sana na alibaini ilikuwa asilimia moja pekee, tena kwa wananchi hasa wanaoishi katika majiji.

Alisema hata Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere katika miaka 63 iliyopita wakati nchi ikipata Uhuru, aliamini na kutoa umuhimu kwenye takwimu katika kupanga mipango ya maendeleo ya nchi, na ndivyo alivyowaridhisha marais waliomfuata

Kamishna wa Sensa na Spika mstaafu, Anne Makinda, alisema serikali imeendelea kutambua umuhimu wa sekta ya nishati katika kukuza uchumi wa nchi kwa kutekeleza mipango na programu mbalimbali za maendeleo kwa kuhakikisha umeme wa kutosha unakuwapo na kusaidia kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kama reli ya kisasa ya SGR na kuzidi kuvutia wawekezaji katika uzalishaji wa bidhaa na huduma na kuimarisha uchumi na maisha ya wananchi.

"Mwekezaji hawezi kwenda kwenye maeneo hayana umeme wa uhakika kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti, Hali ya upatikanaji wa Nishati Tanzania bara kwa mwaka 2019 uliofanywa na NBS kwa kushirikiana na REA ilionesha upatikanaji wa Nishati ulikuwa ni kwa asilimia78.5, mjini ulikuwa asilimia 99.6 na vijijini," alisema Makinda.

Kadhalika utekelezaji wa mpango kabambe wa kupeleka umeme vijijini umewezesha jumla ya vijiji 12,240 kati ya 12,318 vya Tanzania Bara, kufikiwa na umeme hadi kufikia Novemba, mwaka huu na wa bei nafuu na wa kuaminika na nguvu zaidi imeelekezwa kwenye vitongoji.

Kamishna huyo wa Sensa alisema usambazaji wa umeme vijijini utaharakisha utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia ambao umelenga ifikapo 2034 asilimia 80 ya wananchi wawe wanatuma nishati hiyo na kwenda sambamba na jitihada za serikali za kupambana na uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi ya nishati za kupikia zitokanazo na kuni na mkaa.

Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi kutoka NBS, Daniel Masolwa, alisema utafiti huo utafanyika ndani ya siku 30 na kuomba wananchi watakaofikiwa kutoa ushirikiano.

Mwakilishi wa REA mhandisi, Salma Bakari alisema utafiti huu ni wa tatu kufanyika kwa kushirikiana na NBS ukitatajiwa kuleta matokeo chanya kwenye kufahamu uhalisia wa mahitaji na kuyafanyia kazi.

Alisema tangu kuanzishwa kwa REA mwaka 2007 wameweza kutekeleza miradi 428 ilipofikia Juni mwaka huu, ikiwamo inayohusika na Gridi ya Taifa na nje ya Gridi Taifa na kwamba wameendelea kupambana kufikisha nishati safi na bora vijijini na kuhimiza wadadisi kujali shughuli hiyo iliyo mbele ya utafiti kwani matokeo yake yanategemewa sana katika maendeleo ya nchi na mahusiano na wafadhili mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# TPA yapokea meli ya kontena 4,000

**Na Kulwa Mzee**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imeendelea kupokea meli kubwa za mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam ikitokea China yenye uwezo wa kusafirisha zaidi ya kontena 4,000.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, kwenye hafla fupi ya kuipokea meli kubwa ya mizigo inayoitwa EverGreen Line Group, Meneja wa Zimamoto na Usalama wa TPA, Mussa Biboze alisema uwekezaji na uboreshwaji mkubwa uliofanywa katika bandari hiyo umekuwa ukiwavutia wawekezaji pamoja na mawakala mbalimbali wa kampuni za meli kuleta meli zao kupitia bandari hiyo.

"Uwekezaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na Serikali ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia TPA katika Bandari ya Dar es Salaam umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kuvutia kampuni kama EverGreen Line Group kuleta meli yake kwenye bandari yetu," alisema Biboze.

Aidha, alisema miongoni mwa maboresho hayo ni pamoja uwapo wa kamera za ulinzi na usalama za kutosha katika eneo lote la bandari pamoja na kuongezeka kwa crane ambazo zinasaidia kushusha na kupakia makontena ndani ya muda mfupi hivyo kufanya meli isitumie muda mrefu kukaa hapo bandarini tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Alisema mara ya mwisho kampuni hiyo kuitumia bandari ya Dar es Salaam ilikuwa zaidi ya miaka 10 iliyopita, lakini wamerudi tena baada ya maboresho makubwa yaliyofanywa na wawekezaji wakiwamo DP World na Adan International Ports Holding.

"Napenda kukiri kuwa kampuni hizi zinazosimamia gati hizi zimeongeza tija kwa serikali pamoja na kuongeza mapato, lakini pia kuongezeka kwa idadi ya wateja wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam," alisema Biboze.

Biboze alisema ujio wa meli kama hiyo utaongeza mapato kwa TPA na TRA, huku ukitoa fursa kwa madereva wengi zaidi ambao watahitajika kwa ajili ya kusafirisha mizigo iliyopo ndani ya makontena hayo.

Meneja wa Kampuni ya EverGreen Line group Tawi la Tanzania, Mohamed Lotfy alisema hapo awali walikuwa wanaleta mizigo kupitia meli ndogo, lakini hivi sasa wameamua kuja na meli kubwa na hiyo yote ni kutokana na maboresho makubwa katika utoaji huduma yaliyofanyika katika bandari hiyo.

Meneja Kitengo cha Biashara na Mahusiano wa Tanzania East Africa Gateway Terminal Ltd, Donald Talawa alisema ni mafanikio makubwa kupata meli kama hiyo yenye uwezo wa kuchukua kontena nyingi zaidi kwa wakati mmoja.

# Uganda yachota mbinu mafanikio kwenye sekta ya madini Tanzania

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAFANIKIO ya Tanzania katika kubadilisha sekta ya madini yamevutia nchi jirani ya Uganda, mataifa hayo mawili yakikubaliana kuimarisha uhusiano kwa ajili ya maendeleo ya pamoja kupitia ushirikiano wa kimkakati wa kikanda unaoongozwa na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP).

Desemba 3 mwaka huu, kikao cha viongozi waandamizi kilifanyika mjini Dodoma, ambako maofisa wakuu kutoka Wizara ya Nishati na Maendeleo ya Madini ya Uganda, Chemba ya Madini Uganda na wawakilishi wa wachimbaji wadogo walikutana na wataalamu kutoka Wizara ya Madini ya Tanzania na washirika wake.

Lengo la mkutano huo lilikuwa kubadilishana maarifa kuhusu usimamizi na utekelezaji wa sekta ya madini.

Mkutano huo ulikuwa sehemu ya mpango mpana wa kubadilishana maarifa ulioandaliwa na UNDP chini ya Mpango wa Madini ya Maendeleo wa ACP-EU. Mpango huu unatekelezwa barani Afrika na nchi za Caribbean na unalenga kusaidia serikali na wadau kuboresha wasifu na usimamizi wa madini ya maendeleo.

Madini hayo ni pamoja na ya viwanda, vifaa vya ujenzi na mawe ya vipimo, ambayo mara nyingi huitwa madini yaliyopuuzwa.

Yahya Samamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini ya Tanzania, alielezea maendeleo ya nchi katika uchimbaji madini tangu uhuru wake mwaka 1961. Alitaja hatua muhimu katika kuongeza thamani na ushiriki wa sekta binafsi.

Safari hii imehusisha kuanzishwa na kuimarishwa kwa taasisi muhimu kama vile Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia ya Tanzania (GST), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Madini Tanzania (TEITI).

Irene Bateebe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Maendeleo ya Madini ya Uganda, alitoa shukrani kutokana na mbinu za kina walizopewa na Tanzania katika sekta ya madini, hasa jinsi nchi ilivyofanikiwa kusimamia na kuratibu wachimbaji wadogo.

Alisema kuwa watatekeleza kwa mifano hiyo bora ya Tanzania ndani ya sekta ya madini Uganda ili kuleta mabadiliko makubwa.

Irene pia alipongeza UNDP, akisisitiza kuwa imekuwa na mchango mkubwa nchini mwao hasa katika kuwezesha kubadilishana maarifa kati ya nchi na kuongeza juhudi za kujenga uwezo.

Alitambua kuwa nchi hizo mbili zina malengo ya kufanana na hivyo juhudi hizo za kubadilishana maarifa ni muhimu katika kuimarisha mifumo ya kisheria, kukuza maendeleo endelevu katika kanda na kuboresha hali za kazi za wachimbaji wadogo ambao ni sehemu muhimu ya mfumo wa uchimbaji.

Godfrey Nyamrunda, Mratibu wa Kitaifa wa Mpango wa Madini ya Maendeleo wa ACP-EU wa UNDP, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika rasilimali za asili za Afrika kwa ajili ya ukuaji jumuishi na endelevu.


**ZANZIBAR HEALTH RESEARCH INSTITUTE**

87 Binguni Road,
Binguni P.O. Box 1439,
Postcode: 72214, Binguni.
Zanzibar

Tel: +255 (0) 776 264 880
Email: info@zahri.go.tz
Website: www.zahri.go.tz

## JOB ANNOUNCEMENT – RE ADVERTISED

Zanzibar Health Research Institute (ZAHRI) was established under Act No. 5 of 2020 and is one of the key institutions of the Revolutionary Government of Zanzibar. ZAHRI is tasked with conducting health research and overseeing the dissemination of scientific information to enhance and advance various treatment methods and the control of human diseases in the country.

ZAHRI is seeking a qualified candidate from any African Country to fill a three-year contract (renewable) position of a Senior Researcher in health-related fields.

**Job summary**
The Senior Researcher is expected to lead in grant acquisition for strategic health research undertaking, lead multidisciplinary team of Researchers and mentor young researchers in line with ZAHRI's strategic plan.

**Senior Researcher (1 Position)**
**Reports to: Director General**

**Applicant Qualifications:**

i. Should hold a Doctoral degree (PhD) in health related fields from a recognized University
ii. Should have a track record of winning grants as a Principal Investigator (PI) for health research
iii. Should have worked or affiliated with research institutions for at least five (5) years
iv. Should have published at least five (5) papers post PhD in relevant peer-reviewed scientific journals

**Responsibilities:**

i. Acquisition of grants for strategic health research undertaking;
ii. Lead the conduct of approved health research and generate evidence-based results for informing policy and decision making;
iii. Provide mentorship and coaching to young researchers in attaining research competences;
iv. Lead the dissemination of research findings across various platforms, including publishing in peer-reviewed scientific journals and presenting at scientific conferences;
v. Lead the synopsis of permitted health research and identify gaps in meeting national priorities;
vi. Assist the development of the annual research implementation plan;
vii. Contribute in reviewing and creating strategic plans, budgets, and priorities for health research;
viii. Develop collaborative teams within health research between public and private institutions to strengthen and promote human health research;
ix. Perform other duties as assigned by the supervisor.

In addition to an engaging work environment, an attractive remuneration package will be offered to the successful candidate.

**Application Procedures:**

1. Applicants should submit a motivation letter and attach their detailed CV, certified copies of academic certificates (in pdf), birth certificate, and residency ID (if applicable), or a copy of passport and names, address and contacts of three referees.
2. Applications should be sent via email to info@zahri.go.tz, addressed to the Director General, Zanzibar Health Research Institute, Binguni, Zanzibar.
3. The deadline for submitting applications is December 20th, 2024, during working hours.
4. More information is available on the website: **www.zahri.go.tz**.

**Note:**
Application submitted without the required documents will not be considered.

Dr. Mayassa Salum Ally
Director General
Zanzibar Health Research Institute
Binguni - Zanzibar

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika yapo ya kujivunia

**JANA** Tanganyika imesherehekea miaka 63 tangu ilipopata Uhuru wake na kujinasua kutoka utawala wa kikoloni.

Katika kumbukizi ya miaka hiyo Tanganyika ina mengi ya kujivunia kwa kuweza kufanya mambo mengi ya maendeleo.

Tanganyika iliyokuwa wakati wa ukoloni na ya leo ya kujitawala yenyewe imefanya mageuzi katika miundombinu ya barabara, idadi ya shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu imeongezeka.

Katika miundombinu ya barabara imepiga hatua kubwa, kutoka kwenye barabara inayoruhusu gari moja upande mmoja na lingine upande mwingine hadi kuwa na barabara inayoruhusu magari manne kwa upande mmoja.

Kadhalika kuwa na mabasi yaendayo kwa haraka katika Jiji la Dar es Salaam, ambalo lilikumbwa na msongamano mkubwa wa magari barabarani na kusababisha foleni ya watu kukaa saa kadhaa huku muda mwingi wakipoteza kwenye foleni hizo, sasa imepungua katika maeneo ambayo yalikuwa yakikumbwa na changamoto hiyo.

Ingawa mabasi hayo yameanza katika Jiji la Dar es Salaam, lakini katika siku za usoni kwenye majiji ambayo yanaendelea kukua suluhisho la foleni barabarani kupitia mabasi yaendayo kwa haraka litafanikiwa.

Kwa wasafiri wanaotumia barabara kwenda mikoani, tumeanza kuona matunda ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ambayo imepunguza muda wa wasafiri kukaa barabarani saa nane hadi kufikia saa nne.

Wasafiri wanaotoka Dar es Salaam, kupitia Morogoro hadi Dodoma, sasa wanaweza kufanya safari za kwenda na kurudi bila uchovu.

Reli hiyo pia itafupisha safari katika mikoa mingine ambayo itapita na kuwafanya wasafiri wajisikie na furaha wanapotumia njia hiyo ya usafiri.

Haya ni baadhi tu ya maendeleo ambayo yameshuhudiwa katika kipindi cha miaka 63 tangu Tanganyika ilipopata Uhuru wake kutoka kwa wakoloni.

Kwa upande wa elimu, kumekuwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa shule kuanzia za msingi, sekondari hadi vyuo vya elimu ya juu.

Kwa sasa karibu kila kata ina shule ya msingi na wanafunzi wamepata fursa ya kuandikishwa kuanzia elimu ya awali bila malipo, hali iliyofanikisha watoto wengi kupata elimu na kuondoa wimbi la utumikishaji wa watoto wadogo kwa kufanyishwa kazi za ndani kwa sababu ya kukosa elimu.

Vyuo vingi vya elimu ya juu vinapokea maombi mengi ya wanafunzi wanaotaka kujiunga na wengi wao wanapata mikopo ya elimu ya juu ambayo inawapunguzia gharama watoto wenye wazazi wasiokuwa na uwezo wa kuwalipia watoto wao.

Kwa sasa kuna wasomi wengi ambao baadhi yao wakimaliza vyuo wanapata ajira moja kwa moja na wale wasiobahatika, elimu waliyoipata kutoka vyuoni inawasaidia kuanzisha biashara zao na kujiajiri wenyewe na hata kufanikiwa kuajiri wenzao.

Kwa upande wa afya, karibu kila wilaya ina kituo cha afya na zahanati zinazosaidia wananchi kupatiwa huduma za afya zilizo bora na kuwaepusha na kutegemea waganga wa jadi wanapokosa huduma hizo karibu.

Vifo vya wajawazito na watoto wanaozaliwa vimepungua kwa kiasi kikubwa baada ya huduma za afya kusogezwa karibu na kuwezesha kinamama kuhudhuria kliniki kila wakati ili kujua afya zao na watoto wao.

Hili ni jambo la kujivunia sana, jambo la msingi ni kuhakikisha mafanikio yote yaliyopatikana yanatunzwa ili kuendelea kupata maendeleo zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Miaka 63 uhuru imeleta shule tele

**TAIFA** limetimiza miaka 63 ya uhuru uliopatikana Desemba 9, 1961 wakati huo nchi ikiitwa Tanganyika kabla ya kubadilisha jina na kuwa Tanzania, baada ya kuungana na Zanzibar.

Miaka 63 ya uhuru si haba ni ya kujivunia, kutokana na ukweli kwamba Watanzania wameendelea kuwa wamoja kwa kudumisha amani, upendo na mshikamano bila kujali kabila, dini wala itikadi za kisiasa.

Ndani ya miaka 63 ya uhuru yapo maendeleo mengi ambayo nchi imefikia, lakini nizungumzie elimu kwa kuzingatia kwamba baada ya uhuru nchi ilitangaza vita dhidi ya maadui watatu.

Maadui hao ni maradhi, umaskini na ujinga. Ili maadui maradhi na umaskini waweze kuondoka, lazima adui ujinga atokomezwe kwanza kwa kuwapa elimu Watazania ili iwasaidie kuwaondoa maadui hao wawili waliobakia.

Historia inaonesha kuwa wakati Tanganyika inapata uhuru, kulikuwa na shule 3,239 za msingi na 41 za sekondari, lakini jitihada za kuondoa adui ujinga zimeendelea kufanyika hadi kufikiwa kuwa na shule nyingi zaidi.

Kwa sasa kuna shule 8,969,110 za msingi za serikali na nyingine 348, 681 za binafsi, pia kuna sekondari 1,467, 958 za serikali za kidato cha kwanza hadi cha nne na 299, 932 za binafsi.

Vilevile, kuna sekondari 97, 243 ambazo ni za kidato cha tano hadi sita na nyingine 43, 724 za binafsi zinazosaidiana na serikali kutoa huduma ya elimu.

Hali inayoonesha kuwa kuna hatua nzuri imepigwa.

Ndani ya uhuru, kuna kasi kubwa kuboresha elimu kwa kujenga shule nyingi za msingi na sekondari ambapo karibu vijiji vyote kila kimoja kina shule mbili za msingi ili kuweza kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Wakati kila kijiji kikiwa na shule mbili za msingi, kwa sasa jitihada nyingine zinafanywa na wananchi kwenye baadhi ya maeneo kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na sekondari yake.

Serikali ilianzisha utaratibu wa kila kata kuwa na sekondari, lakini sasa wananchi nao wamejiongeza kwa kupiga hatua kwenda mbele na sasa wameanzisha utaratibu wa kila kijiji kuwa na sekondari yake.

Hatua hiyo inalenga kuwapunguzia watoto wao changamoto za kusafiri umbali mrefu kufuata elimu, pia hatua hiyo inakusudia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika madarasa.

Kwa mfano, baadhi ya kata zina vijiji zaidi ya vitatu na wakati mwingine viko mbali na eneo ambalo iko sekondari, matokeo yake wanafunzi wanalazimika kusafiri umbali mrefu kwenda shule.

Penye mafanikio pana changamoto zake. Ni kweli miaka 63 ya uhuru, nchi imepiga hatua kwenye elimu kwa kuongeza idadi ya shule, lakini ipo changamoto ambayo ni vyema ikatatuliwa ili kuboresha elimu.

Shule zipo, nyingine zinaendelea kujengwa, ila ukosefu wa walimu wakiwamo wa masomo ya sayansi, ukosefu wa wataalam wa maabara unaweza kukosesha nchi wataalam wa fani mbalimbali wa baadaye.

Changamoto haiishii hapo tu, bali pia ipo ya ukosefu vyumba vya madarasa, madawati, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukosefu wa mabweni ambavyo vyote ni hatari kwa ustawi wa elimu.

Hivyo, tunaposheherekea miaka 63 ya uhuru, tujivunie wingi wa shule tulizonazo sasa baada ya nchi kupata uhuru, lakini pia tukitafakari jinsi ya kuziboresha ili ziweze kusaidia kuinua ubora wa elimu.

Lengo ni kutaka kupata elimu bora, si bora elimu. Hivyo wadau wa elimu wakae na kutafakari ili wahakikishe hakuna uhaba wa walimu, wataalam wa maabara na vitu vingine vya muhimu vipasavyo katika ujifunzaji na ufundishaji.

TOLEO MAALUM

MAADHIMISHO YA MIAKA 80 YA USAFIRI WA ANGA DUNIANI

# TCAA CCC: Tanzania Kinara wa Mfumo wa Kumtetea Mtumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga barani Afrika

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zenye mfumo kwa ajili ya kumlinda na kumtetea mtumiaji wa huduma za Anga. Uanzishwaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC) kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 kunaifanya Tanzania kuwa nchi pekee Afrika kuwa na taasisi mahsusi kwa ajili ya kumlinda, kumtetea na kumsemea mtumiaji wa huduma za usafiri wa anga.

Majukumu haya katika nchi nyingine barani Afrika yamekuwa yakikasimishwa ama katika kitengo chini ya Wizara yenye dhamana ya uchukuzi, au kitengo chini ya Mamlaka za udhibiti wa usafiri wa anga au wakala wa kumlinda mtumiaji kutoka katika sekta zote na katika baadhi ya nchi kutokuwepo kabisa kwa taasisi ya Serikali inayomlinda mtumiaji wa huduma za usafiri wa anga.

Hatua hii ya uwepo wa TCAA CCC kunaonesha dhamira ya Serikali ya Tanzania ya kuimarisha uwajibikaji, uwazi, na ufanisi wa sekta ya usafiri wa anga kwa kutambua mchango wa watumiaji wa huduma hiyo katika kuendeleza sekta ya usafiri wa anga hivyo kuchangia ukuaji wa Uchumi wa nchi yetu.

Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) za mwaka 2023, sekta ya usafiri wa anga inachangia asilimia 2.5 katika pato la taifa, ikiongezeka kutoka asilimia 0.8 mwaka 2018.

Sekta hii kama zilivyo sekta nyingine inaongozwa na watumiaji kwa sababu ndiyo wanaamua kampuni gani ya kutumia kwa ajili ya safari za ndani na nje ya nchi. Kumbukumbu zinaonesha kwa mwaka hadi kufikia mwezi Juni, 2024 zaidi ya abiria 5,797,000 walikua wametumia viwanja vya ndege vilivyopo nchini.

Watumiaji wa huduma za usafiri wa anga wanajumuisha wasafiri wa kibiashara, watalii, wafanyabiashara, wanadiplomasia na wananchi wa kawaida wanaotumia usafiri huu kwa sababu mbalimbali.

Tunapoadhimisha miaka themanini (80) ya Usafiri wa Anga Duniani pamoja na miaka sabini na tano (75) ya uwezeshaji watumiaji wa huduma ya usafiri wa anga, haki za abiria zinapaswa kuwa kipaumbele cha kwanza.

Abiria wanapaswa kupata taarifa sahihi kuhusu haki zao, kama vile fidia kwa ucheleweshaji au kufutwa kwa safari, huduma zisizoridhisha au upotevu wa mizigo.

Kampeni za uhamasishaji na elimu kuhusu haki hizi zinaweza kusaidia abiria kufahamu wanachostahili na jinsi ya kudai haki zao kwa njia iliyo rasmi.



Bw. Innocent Kyara, Katibu Mtendaji wa TCAA CCC

TCAA CCC imekua ikitoa elimu kwa umma kwa kutumia tovuti, mitandao ya kijamii, kushiriki katika maonesho ya wazi kama Sabasaba na Nanenane, kuandaa vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari, kuendesha warsha kwa wadau na kuandaa program za mafunzo ya huduma kwa wateja katika viwanja vya ndege.

Aidha, ubora wa huduma pia unapaswa kuzingatiwa kwa kina. Mashirika ya ndege yanapaswa kuhakikisha huduma zao zinakidhi viwango vya kimataifa. Mifumo ya kushughulikia malalamiko inapaswa kuwa ya haraka, shirikishi na inayotatua changamoto za abiria kwa haki.

Kuundwa kwa TCAA CCC kumeleta mapinduzi makubwa katika kuwawakilisha abiria na kushughulikia malalamiko yao dhidi ya watoa huduma wa usafiri wa anga.

Huduma hii inahusisha kutoa msaada wa kisheria na kuwawakilisha abiria katika mashauri ya kisheria dhidi ya watoa huduma katika mfumo wa utatuzi wa malalamiko uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Anga.

Huduma hizi hutolewa na TCAA CCC kwa abiria wenye malalamiko bila malipo, hivyo kuwaepusha abiria wa usafiri wa anga na mzigo mkubwa wa gharama za kisheria na muda wa kufuatilia haki zao katika vyombo vya kisheria.

Usalama wa abiria ni eneo ambalo haliwezi kupuuzwa pamoja na ukweli kuwa nchi yetu imekuwa na matukio machache sana yanayotishia usalama wa abiria, hali hii isitufanye tukabweteka.

Uwepo wa mifumo madhubuti wa kuzuia matukio hayo kabla hayajaleta madhara kwa abiria ni muhimu ukaendelea kusimamiwa kwa ukaribu kama inavyofanyika hivi sasa.

Mamlaka zinapaswa kushirikiana na kuimarisha viwango vya kiusalama katika viwanja vya ndege na ndani ya ndege.

Hii inajumuisha kuhakikisha mashirika yote ya ndege yanazingatia viwango vya kimataifa vya usalama, sambamba na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa sekta hiyo ili kuboresha uwezo wao wa kushughulikia hali ya dharura.

Mwezi Mei 2023, Tanzania ilikaguliwa na Shirika la Kimaitaifa la Usafiri wa Anga (ICAO) na kuwa nchi ya nne kwa kufikisha alama 87% katika ukaguzi wa usalama wa usafiri wa anga (ICAO aviation security audit). Hatua hii itaendelea kujenga imani ya abiria katika huduma za usafiri wa anga nchini.

Katika hatua nyingine, ni maoni ya TCAA CCC kuwa ufikiaji wa huduma za anga kwa wote ni suala muhimu kwa maendeleo jumuishi. Kwa kuzingatia ukubwa wa jiografia ya nchi yetu, ni muhimu kukawepo na mikakati ya kufanya usafiri wa anga kuwa nafuu (affordable) hivyo kufanya kuwafanya watu wengi zaidi kumudu njia hii ya usafiri na kupunguza matumizi yaliyopitiliza katika njia nyingine ya usafirishaji.

Katika nyanja ya mazingira, sekta ya usafiri wa anga inapaswa kujitahidi kupunguza athari zake kwa mazingira. Mashirika ya ndege yanaweza kuhamasishwa kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira, kama ndege zinazotumia nishati mbadala au zinazotoa hewa chache ya ukaa pamoja na kelele ndogo.

Hatua hizi zitasaidia katika juhudi za kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kuimarisha mifumo ya kidigitali na utoaji wa habari ni muhimu pia. Taarifa kuhusu ratiba na mabadiliko ya safari zinapaswa kupatikana kwa urahisi na kwa uwazi.



Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof. Makame Mbarawa akipokea pongezi kutoka kwa Katibu Mtendaji wa TCAA CCC Bw. Innocent Kyara, mara baada ya kukamilisha kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi ya mwaka 2024/25 Bungeni Jijini Dodoma.

Hii itasaidia abiria kupanga safari zao kwa ufanisi zaidi na kuepuka gharama, ambazo mara nyingi husababisha usumbufu mkubwa.

TCAA CCC imekuwa nguzo muhimu katika kulinda haki za watumiaji wa usafiri wa anga nchini kwa kufanya usimamizi wa haki, ufuatiliaji wa huduma, kukusanya maoni na kushirikisha wadau,

Ushirikiano wa kikanda na kimataifa ni muhimu kwa kuboresha sekta ya usafiri wa anga. Nchi na mashirika ya kimataifa yanapaswa kuendelea kushirikiana katika kuhakikisha viwango vya juu vya huduma na uwajibikaji mashirika ya ndege.

TCAA CCC imekua na ushirikiano na Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika (AFCAC), taasisi watumiaji wa usafiri wa anga Afrika Mashariki na taasisi nyingine za kimataifa zenye malengo yanayofanana na shughuli za baraza.

Ushirikiano huu unalenga kubadilishana uzoefu na mikakati ya kuendelea kumlinda na kumtetea mtumiaji wa huduma za usafiri wa anga

Baraza linaendelea kuhakikisha kwamba huduma za usafiri wa anga zinaendeshwa kwa uwazi kwa maslahi ya mtumiaji na sekta nzima kwa ujumla.

Ni jukumu la kila mtumiaji pia kuhakikisha anajua haki zake na kuzidai inapobidi, au kuomba kupata usaidizi kutoka TCAA CCC.

Pamoja na ufinyu wa rasilimali, tunajivunia kuendelea kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma ya usafiri wa anga kwa kutoa taarifa na maoni muhimu kuhusu masuala mbalimbali kwenye usafiri wa anga.

Kwa kuhitimisha, pongezi kubwa tunazielekeza kwa Serikali chini ya Uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa na muhimu katika sekta ya usafiri wa anga ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege, ikihusishwa ujenzi wa majengo ya abiria, njia za kurukia ndege na mifumo mbalimbali ya kuongozea ndege.

Maboresho haya yatavutia uwekezaji na kuongeza ushindani wa soko hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Aidha, tunaamini maadhimisho haya ni fursa nzuri ya kutathmini mafanikio na kuweka mikakati endelevu kwa manufaa ya abiria na wadau wote wa sekta ya usafiri wa anga.

Watumiaji wa huduma za usafiri wa anga na umma kwa ujumla wanaweza kuwasiliana na Baraza la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC) kwa elimu na ufafanuzi zaidi wa masuala mbalimbali kuhusu usafiri wa anga kupitia mitandao yetu ya kijamii ya Instagram **(@tcaa_ccc), Mtandao X (@tcaa_ccc1) na Youtube (@TCAA_Consumer_Consultative_Council) au kupiga simu ya bure nambari 0800 110 190 au kupitia anuani iliyoainishwa hapa chini;**

**Katibu Mtendaji,**
**Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC)**
**Majengo ya TBA Na. L1,**
**Kiwanja Na. 6/2,**
**Mtaa wa Kilimani, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,**
**S. L. P 12242,**
**14110 DAR ES SALAAM**



Mwonekano wa Jengo la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato litavyokuwa pindi ujenzi utakapokamilika mwishoni mwa mwaka 2025.





Ujenzi wa Jengo la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ukiendelea wakati TCAA CCC ilivyotembelea mradi huo Novemba, 2024.

# Waanika kiini Nyanda za Juu Kusini kuongoza mimba, ndoa za utotoni

**Na Moses Ng'wat,**
SONGWE

WADAU kutoka makundi mbalimbali wamekutana katika mdahalo kujadili na kujengeana uelewa kuhusu dhana halisi ya ukatili wa kijinsia na madhara yake katika jamii, ikiwa ni pamoja na kupata uzoefu kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya mkoa wa Songwe.

Mdahalo huo ulifanyika mwishoni mwa wiki na kuhudhuriwa na wadau kutoka makundi mbalimbali, viongozi wa dini na mila, asasi za kiraia, viongozi wa Jeshi la Polisi na kusimamiwa na mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Songwe, John Mwaijulu.

Akifungua mdahalo huo uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa huko Nselewa, Wilayani Mbozi, mwakilishi huyo wa Katibu Tawala alisema kuwa mdahalo huo unatoa fursa ya kujadili changamoto ya mimba katika umri mdogo, ikizingatiwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo inayoongoza kwa kuwa na changamoto kubwa ya mimba katika umri mdogo na Songwe ndio unaongoza kitaifa kwa asilimia 45.

"Matarajio yetu kama mkoa ni kuona washiriki wote mlioalikwa mnatoa michango chanya inayolenga kusukuma mbele jitihada za kukabiliana na ukatili wa kijinsia na mimba katika umri mdogo," alisema.

Mkurugenzi wa Jinsia kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Badru Abdununi, akitoa takwimu za ndoa na mimba za utotoni katika mdahalo huo, alisema zinaonesha kuwa mikoa ya nyanda za juu kusini ya Songwe, Ruvuma, Katavi na Rukwa ni miongoni mwa mikoa mitano inayoongoza nchini kwa ndoa na mimba za utotoni, ukiacha mkoa wa Mara ambao uko nje ya kanda hiyo.

Abdununi alisema kuwa kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2023, mkoa wa Songwe ndio unaongoza ukiwa na asilimia 45, ukifuatwa na Ruvuma wenye asilimia 37, Katavi ni wa tatu ukiwa na asilimia 34, Rukwa inashika nafasi ya tano ukiwa na asilimia 30 huku mkoa wa Mara ukiwa ni wa nne kwa asilimia 30 pia.

Miongoni mwa wadau waliochangia katika mdahalo ni Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wazee Mkoa wa Songwe, David Songolo, aliyesema kuwa miongoni mwa mambo yanayochangia ukatili huo wa ndoa na mimba za utotoni ni malezi mabovu ya familia.

Songolo alisema wanaume wengi katika mkoa wa Songwe na mikoa jirani wamekuwa wanaendekeza tabia na mila za kuoa wake wengi, jambo linalichangia malezi mabaya.

Songolo alisema mila na desturi ya kuwa na wake wengi huwa haiendani na uchumi wa familia, hivyo kusababisha kushindwa kukidhi mahitaji ya familia na watoto kukosa ulinzi na kujikuta wakiangukia kwenye vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Songolo alipendekeza marekebisho ya sheria na kutaka sheria kuwatambua wazee na viongozi wa mila kuwa sehemu ya kusimamia malezi na maadili ya kitanzania.



Waziri Mkuu Mstaafu ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Mizengo Pinda (Kulia), akimpongeza Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Njombe, Scholastica Kevela, baada ya kumtunuku Shahada ya Uzamivu katika masuala ya Fedha wakati wa mahafali yaliyofanyika mkoani Kigoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

**Na Tuntule Swebe**

MTOTO Joshua Tarimo (11) pichani chini, ametoweka nyumbani kwa mlezi wake Tandale Kwatumbo, Dar es Salaam tangu Desemba 5, mwaka huu.

Mlezi wa mtoto huyo, Salama Salimu, akizungumza na Nipashe jana alidai kuwa mwanawe huyo alitoweka Desemba 5 mwaka huu asubuhi.

"Niliangalia fedha zangu mahali ninapoweka sikuziona. Baada ya kufuatilia kwa kina, nilihisi mwanangu ndiye kazichukua, nilimwuliza mwanangu aitwaye Asma Mohamed (21) na Joshua.

"Katika kuwahoji ilibainika Joshua ndiye kazichukua fedha hizo na kumtaka azirudishe, ndipo aliamua kuondoka kwenda kusikojulikana kwa kuhofia kupewa adhabu.


"Saa chache ndipo nilipogundua kuwa Joshua hayupo nyumbani, nilimtafuta sikumpata ndipo nilipochukua jukumu la kumwambia mama yake.

"Nilipojaribu kumwuliza mama yake, alisema mtoto huyo hakuwa kwake, tulimtafuta kwa ndugu wa karibu, lakini hatukumpata," alisema.

Salama alisema wameshatoa taarifa kituo cha polisi na kufungua faili namba MBT/RB/6328/2024.

"Ninaogopa sana huyu mwanangu asikumbwe na jambo baya, kwa sasa kuna matukio ya watu kupotea na kutekwa, nina hofu sana, kokote aliko arudi nyumbani," alisema.

Alisema kuwa siku hiyo alikuwa amevaa fulana ya rangi ya chungwa na suruali ya rangi ya kijivu na yeboyebo za rangi ya kijani. Atakayemwona awasiliane na mama huyo kwa namba 0684304142 au 0719058662.



# ...Kutoripoti uhalifu chanzo ongezeko la ukatili kwa wanawake na watoto

**Na Mussa Mwangoka,**
MPANDA

MWAMKO mdogo wa wananchi kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto umetajwa kuwa moja ya sababu zinazochangia ongezeko la vitendo hivyo kila kukicha katika mkoa wa Katavi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, SACP Kaster Ngonyani aliyasema hayo jana baada ya kutembelea na kutoa misaada katika Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika, ikiwa ni sehemu ya kuwafariji wagonjwa kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

SACP Ngonyani alisema vipo visa vingi vya ukatili wa kijinsia ambavyo vimekuwa vinatokea, ukiwamo ubakaji, ulawiti, vipigo na mimba kwa wasichana wenye umri mdogo, lakini haviripotiwi katika vituo vya polisi wala kwenye vyombo vya habari, hali inayofanya vitendo hivyo kuendelea kushamiri katika jamii.

"Tujitokeze tutoe taarifa za siri kuhusu uhalifu, na turipoti vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, watoto na wanaume kuliko kukaa kimya. Tunaelewa kuna visa vingi vinatokea ila miongoni mwetu hatutaki kuripoti polisi.

Ninashauri tuache hiyo tabia kwani kuripoti kunasaidia kumaliza changamoto hii," alisema.

Kamanda huyo alisema kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu kuhusu kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, likitumia makundi mbalimbali kama kuwafikia wanafunzi, wazee, kinamama na vijana ili kupunguza visa hivyo.

Dk. Daniel Mwansembo, Kaimu Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wilaya Tanganyika alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba mwaka huu wamehudumia wagonjwa wasiozidi 20 waliofanyiwa vitendo vya ukatili, zikiwamo mimba za utotoni.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko alionya kuhusu ongezeko la vitendo vya ukatili ambavyo vinachangia kuwapo mimba na ndoa za utotoni, akiagiza makundi yote katika jamii kushirikiana na serikali kudhibiti hali hiyo.

"Masuala ya ubakaji, ulawiti, mapenzi ya jinsia moja, mimba za utotoni na migogoro ya kijamii, yote ndani ya mkoa wetu yapo na yanatokea na yanaongezeka. Kila mmoja kwenye nafasi yake analo jambo la kufanya ili kudhibiti matukio hayo," aliagiza.

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya Mwaka 2022 inataja mkoa wa Katavi kuwa wa tatu kitaifa kwa mimba na ndoa za utotoni ukiwa na asilimia 34, nyuma ya Songwe wanaoongoza kitaifa kwa silimia 45 na Ruvuma wanaoshika nafasi ya pili kwa asilimia 37.



# Wanafunzi kunywa uji wa mtama kuimarisha afya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema serikali inakuja na mkakati mahususi utakaochagiza wanafunzi mkoani hapa kunywa uji wa mtama kila siku, kutokana na kuwa na viini lishe vingi.

Alisema hayo juzi katika fainali za mashindano ya lishe yaliyowahusisha wanafunzi wa shule za sekondari 93.

Babu, alisema ukichunguza afya za watu wanaopata matatizo mengi ya kiafya, unagundua shida kubwa ni kukosa viini lishe ambavyo vingi vipo kwenye zao la mtama.

Mashindano hayo ya lishe yaliandaliwa na Shirika la Floresta Tanzania, kwa kushirikiana na Shirika la World Vegetable Center, kupitia Mradi wa Kupeleka Teknolojia Haraka kwa Wakulima (AID-I), unaofadhiliwa na Marekani.

"Nikiwa DC kule Kilwa (Mkuu wa Wilaya), niliacha legacy (alama) kwa kuagiza kila shule kuwa na ekari tano za kulima mtama, matunda na mboga kwa ajili ya lishe. Sasa huku Kilimanjaro, ardhi ni tatizo lakini kama viini lishe vyake vingetumika ipasavyo, vingekuwa na uwezo mkubwa wa kutatua changamoto za afya ya Watanzania na kuzuia wanafunzi wetu kupata changmoto za afya kama utapiamlo," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Floresta Tanzania, Richard Mhina, alisema kupitia mradi huo, wamejizatiti kuhamasisha matumizi ya mlo kamili unaojumuisha mboga na matunda, kwa lengo la kupambana na changamoto za lishe duni miongoni mwa jamii, hasa kwa vijana balehe.

"Mashindano haya yanahusisha shule nane zilizofuzu kutoka awamu mbili zilizopita, na yanalenga kuimarisha uelewa wa lishe bora, uzalishaji na matumizi ya mboga, kwa njia shirikishi kupitia mada fupi na midahalo.

"Fainali hizi zinahitimisha mchakato wa awamu tatu za mashindano yaliyolenga kutoa elimu ya lishe shuleni. Awamu ya kwanza, ilihusisha ngazi ya kata, ambapo jumla ya shule 93 zilishiriki, huku awamu ya pili kwenye ngazi ya wilaya ikishirikisha shule 50.

...Hatua ya mwisho, inalenga kupima uelewa wa wanafunzi na walimu kuhusu umuhimu wa lishe bora, uzalishajiwa mboga na matumizi yake kwa afya bora. Mradiwa AID-I, unalenga kurahisisha upatikanaji wa mbegu na miche bora ya mboga kwa wakulima, kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya mboga, matunda, na viungo, pamoja na kuboresha lishe ya jamii."

Aidha, mashindano hayo yalienda sambamba na kampeni za kuhifadhi mazingira, ambapo Floresta Tanzania inashiriki maadhimisho ya kimataifa ya CNN Call to Earth Day yanayofanyika kila Desemba.

Floresta Tanzania kupitia kampeni hiyo, inalenga kupanda miti 500,000 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu kwa kushirikiana na shule, familia za wakulima na wadau wengine wa maendeleo.

## Gharama uagizaji mafuta nje kupungua

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI imesema mradi wa utafiti wa uchimbaji na uzalishaji wa mafuta ghafi katika eneo la Eyasi-Wembere lililopo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, utaipunguzia Tanzania mzigo wa gharama za kuagiza mafuta hayo nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mradi wa Utafiti wa Mafuta katika Bonde la Eyasi-Wembere, Sindi Maduhu, hatua iliyofikiwa Tanzania ina matumaini makubwa ya kugundua mafuta kutokana na rasilimali hiyo kupatikana maeneo mengine ya bonde hilo.

Maduhu, alidokeza matumaini hayo wakati wa mkutano wa watafiti na wasayansi kutoka ndani na nje ya nchi uliofanyika jijini Tanga.

Alisema: "Huu utafiti unaendelea katika Bonde la Eyasi-Wembere lililopo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki. Uzalishaji utakapoanza rasmi tuna amini utachangia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa taifa, kwa kuongeza pato la taifa na kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje".

Bonde la Eyasi-Wembere, linapita katika mikoa mitano ya Shinyanga, Simiyu, Arusha, Singida na Tabora.

Inaelezwa kwamba, Eyasi-Wembere ina uhusiano wa kipekee na maeneo mengine ya Bonde la Ufa, upande wa mataifa ya Uganda na Kenya, ambako nchi hizo tayari zimegundua mafuta.

"Eneo hili ni muhimu sana kwa Tanzania kutokana na mshikamano wake na maeneo ya Lokicha nchini Kenya, ambapo mafuta yamevunjwa, na Uganda, ambapo wanajenga bomba la mafuta ghafi ili kupeleka mafuta hayo kwenye viwanda vya usafirishaji," alisema Maduhu.

Kuhusu maendeleo ya utafiti huo, Maduhu alisema kazi za utafiti ziko katika hatua nzuri tangu kuanza kwa mradi huo mwaka 2015.

Alisema hadi sasa wamefanikiwa kukusanya taarifa muhimu zinazohusiana na uwepo wa mafuta katika eneo hilo.

Alisema kuwa katika hatua hii, wanatekeleza uchukuaji wa taarifa za mitetemo ya mifumo ya 2D ili kubaini maeneo ya kuchimba, kwamba kila awamu ya utafiti, inahusisha watu 200, ambapo zaidi ya asilimia 90 ya wafanyakazi ni Watanzania.




Mganga mkuu wa wilaya ya Muheza Tanga Fani Mussa Kulia jana akionyesha bango katika Hospitali ya Teule iliyopo wilayani Muheza Tanga ambayo inamilikiwa na kanisa la Anglikana Tanzania iliyofunguliwa na baba wa Taifa hayati Julius Kambarage Nyerere Tarehe 15/Julai/1981katika maadhimisho ya miaka 63 ya uhuru wa Tanzania bara yaliofanyika kiwilaya kwa kufanya usafi wa mazingira na kutoa zawadi kwa wagonjwa hospitali hiyo mgeni rasmi mkuu wa wilaya Zainabu Abdallah. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ukatili mpya waibuka Mwika Kaskazini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWENYEKITI wa Kijiji cha Lole, Kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, John Safiel, amesema aina mpya ya ukatili unaoitesa jamii katika eneo hilo kwa sasa ni wanaume walioko kwenye ndoa kuandaliwa maji ya kuoga bafuni na watoto wao wa kike.

Alisema hayo juzi wakati wa mdahalo wa kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kama sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili.

Safiel alieleza namna kundi hilo la wanawake walioko kwenye ndoa, linavyoweka kando jukumu lao na kuwatwisha zigo hilo watoto wao hasa wa kike.

"Hapa kwetu Mwika, baadhi ya wanawake wamesahau wajibu wao kwa waume zao kama vile kuwapikia, kuwapashia maji na kuwapelekea bafuni; badala yake wanawatwisha watoto wao kazi, ambazo walitakiwa wazifanye. Sasa jambo hili linachangia kuchochea ukatili dhidi ya watoto," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Safieli, alisema Serikali ya Kijiji inaendelea kushirikiana na Shirika la KWIECO, kupinga vitendo vya kikatili dhidi wanawake na watoto, huku akiwataka wanaume kusimama katika nafasi zao kwa kuwajibika kuhudumia familia.


Alisema anawaunga mkono wanawake kwa kuwa wamekuwa wakishiriki katika maendeleo ya kijiji hicho, huku akieleza namna KWIECO lilivyogeuka chachu ya mabadiliko makubwa katika masuala ya haki za wanawake, watoto na uchumi.

Mmoja wa wanawake wa kijiji hicho, Salome Shao, alisema kumekuwepo na mabadiliko makubwa katika jamii ya kichaga, kwa vile mwanamke sasa anashiriki katika fursa za kiuchumi, hususani kutoa maamuzi katika masuala mbalimbali kama vile ujenzi na shughuli nyinginezo za maendeleo.

Exaud Shao, alisema kutokana na wanawake kuwa na uchumi mkubwa, huku wanaume wakiwa na vipato duni, kunasababisha ndoa nyingi kuvunjika na watoto kuishi katika mazingira hatarishi, kwa kukosa malezi ya wazazi pande zote mbili.

Mratibu wa mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT), Veronica Ollomi, alisema moja ya mambo ambayo yanatikisa kwa sasa katika jamii ya Kilimanjaro ni makosa ya ukatili wa kingono.

Alisema: "Ukatili wa kingono, ni tendo lolote la kingono kama vile kugusa, kubusu, kusugua, au kujamiana, ambako kunatokea bila idhini. Hii ina maanisha mwathirika hakukubali kufanya hivyo na alilazimishwa, alidanganywa, au kuendeshwa kufanya".





# Maswi: Utoaji wa haki mahakamani bado hauridhishi

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Eliakim Maswi amesema licha ya idara zote chini ya wizara hiyo nchini kuelekezwa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, bado utoaji wa haki katika baadhi ya mahakama nchini hauridhishi.

Maswi alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe na kutaja hali hiyo kuwa zaidi katika baadhi ya mahakama za mwanzo kutokana na upungufu mbalimbali ikiwemo wa watumishi na baadhi ya mahakama kuwa mbali na maeneo ya makazi ya wananchi.

Alisema mahakama hizo zinakabiliwa pia na uchakavu wa majengo pamoja na upungufu wa watumishi wakiwemo mahakimu na makarani hali aliyoitaja kukwamisha utolewaji haki kwa wakati.

Alisema katika usimamizi wa mapendekezo ya tume hiyo, shughuli za kila siku za mahakama zimeboreshwa ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao kwa wakati na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na tume hiyo.

"Tunatekeleza kwa vitendo maagizo ya tume iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha tunatokomeza vikwazo vyote vinavyozuia upatikanaji haki kwa wananchi kwa wakati katika vyombo vya sheria," alisema Maswi.

"Jitihada za kukabiliana na upungufu huo ni pamoja na kuomba kuongezewa bajeti kwa ajili kuajiri watumishi wapya sanjari na kujenga mahakama zinazoweza kufikika kirahisi hasa maeneo ya vijijini na pembezoni," alisema.

Aidha, alisema wizara hiyo inaendelea kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusu kupata hukumu kwa lugha ya kiswahili kutoka katika lugha ya kiingereza kwa kuanzisha mfumo wa unukuzi na tafsiri ambao pia unawasaidia majaji na mahakimu kuendesha mashauri bila kuandika kwa mkono.

Maswi alisema mwanzoni mwa mwaka 2025 anatarajia kufanya ziara katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kukagua na kujionea utekelezaji wa mapendekezo ya tume hiyo ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao kwa wakati.

Rais Samia Suluhu Hassan aliunda tume hiyo Januari 2023 ikiwa na wajumbe tisa kupitia na kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo wa taasisi za haki jinai nchini kazi iliyokamilika na kuwasilishwa mwezi Julai 2023.

Baada ya kupokea mapendekezo ya tume hiyo yaliyolenga kuboresha taasisi za haki jinai, Rais Samia aliibadilisha tume hiyo na kuwa Kamati ya Kusimamia Utekelezaji na kusaidia serikali kuandaa mpango wa utekelezaji wa mapendekezo hayo.



Mkuu wa wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro (kushoto) akipima maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwenye maadhimisho ya miaka 63 ya uhuru wa Tanganyika **PICHA: MARCO MADUHU**

# UN yarejesha eneo lililotumika kuwapa chakula wakimbizi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limeikabidhi rasmi serikali eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 29,450 la kituo cha kimkakati kilichotumika kugawia chakula cha msaada kwa wakimbizi wa nchi za ukanda wa magharibi.

Kituo hicho kilichopo Isaka wilayani Kahama mkoani Shinyanga kilitolewa na Serikali ya Tanzania kwa shirika hilo Januari, 1996 na mwaka 2004 serikali ilithibitisha kwa barua kulipokea na kukabidhiwa rasmi juzi 2024.

Naibu Mkurugenzi wa WFP, Christine Mendes akikabidhi eneo hilo juzi kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Hamadi Mbega alisema kuwa kituo hicho kilitumika kusambaza chakula cha msaada kwa wakimbizi ambapo chakula hicho kilikuwa kikisafirishwa kutoka Bandari ya Dar-es Salaam kupitia reli ya kati.

Alisema chakula walichokuwa wakisambaza katika nchi za Rwanda, Burundi, DRC, Kenya, Sudani Kusini na Uganda ni pamoja na maharage, mahindi na mtama.

"WFP ilijenga bure kituo hiki na kuweka mtandao wa miundombinu ya reli mbili za kutoka Stesheni ya Isaka hadi kwenye kambi hii yenye umbali wa mita 1200 , tuliweka maghala 54 ya kuhamishka, uzio, nyumba mbili za watumishi na mashine," alisema Mendes.

Katibu Tawala Wilaya, Mohamed Mbega alisema tayari wamepokea eneo hilo baada ya WFP kumaliza kazi zao na kuwa serikali itakaa kujadilili ni taasisi ipi ipewe eneo hili ili kutekelea shughuli zake.

Meneja wa Shirika la Reli Kanda ya Tabora, John Mamuya alisema eneo hilo walipendekeza wapatiwe kwa sababu hata katika ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) watalitumia kuhifadhi vifaa na ikikamilika litumike kuweka mizigo inayotarajiwa kusafirishwa.

Diwani wa Kata ya Isaka, Pazi Majuta alisema asilimia 70 ya uchumi wa Isaka ulijengwa na WFP na wao walikaa kwenye halmashauri na kujadiliana kuhusu eneo hilo na kupendekeza lilirudi kwenye kijiji ili waliendeleze kwa kuweka miundombinu kama shule.

# Wapanda miti 230,000 kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru

**Na Daniel Limbe,** CHATO

KATIKA kuadhimisha sherehe za miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara, wananchi wilayani Chato mkoani Geita wameshiriki kufanya usafi na kupanda miti 230,000, lengo likiwa ni kuhifadhi mazingira dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza wakati wa upandaji wa miti hiyo katika eneo la Hospitali ya Wilaya hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Christian Manunga alisema wamepanda miti 230,000 katika Kata 23 wilayani humo ikiwa ni sehemu ya kutimiza agizo la upandaji wa miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri kila mwaka.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Thomas Dimme, aliwataka wananchi kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti kila kaya, kufanya usafi, kunawa mikono pamoja na kutumia vyoo bora ili kulinda afya zao.

Pia, alizitaka taasisi binafsi na za umma kupanda na kutunza miti kwa manufaa ya sasa na baadaye na kwamba ni aibu kwa nchi kama Tanzania kugeuka jangwa licha ya kuwa na ardhi bora na yenye rutuba nzuri kwa mimea na mazao.

Katibu wa CCM Wilaya, Charles Mazuri alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kipindi chote cha uhuru wa Tanzania Bara bado vita ya Kagera na Uganda imebaki kuwa chanzo kikuu cha kutofikia uchumi mkubwa ukiliganisha na nchi nyingine.

"Kama siyo vita hiyo naamini sasa hivi tungekuwa mbali sana kiuchumi kama walivyo wenzetu China, maana baada ya vita ile nchi yetu ilifilisika kiasi kwamba baadhi yetu tulilazimika kufua nguo kwa kutumia magome ya miti,"alisema Mazuri.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mandia Kihiyo, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Chato inaendelea kutekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa lengo la kuinua ustawi wa wananchi na kuboresha maisha ya kila mtanzania kutokana na mipango madhubuti ya serikali.

Mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) wilayani hapa, Peter Mwadima, alisema wanaendelea kusisitiza jamii kutunza mazingira kwa kutoharibu misitu ya hifadhi kutokana na shughuli za kibinadamu, badala yake kila mwananchi aone thamani ya kupanda na kutunza miti.

Kadhalika alisema kwa wilaya hiyo wameotesha miche zaidi ya 200,000 ambayo ipo tayari kwa ajili ya kupandwa maeneo mbalimbali ya jamii, huku wananchi na taasisi zikialikwa kuchangamkia fursa hiyo.



Ukurasa 12

**Kinachohitajika ni kurejesha rasilimali kwa Watanzania**

**+63 BAADA YA UHURU**

Tanzania iinuke kufikia miaka 100 ya uhuru iking'ara zaidi


Ukurasa 13


Ukurasa 14

**Kumbukizi za masuala ya Uhuru**


Nipashe TESA

Jumanne Desemba 10, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


ELIMU NA SABATO KASIKA

SHUJAA LAWI SIJAONA

# Mpigania uhuru aliyemkaribisha Mwalimu Nyerere kwenye vyama

- Alibwaga ajira, akazama ndani ya siasa
- Ni msimamizi kamati iliyoandaa katiba

YAWEZEKANA ni jina geni kwa baadhi ya watu hasa wa kizazi kipya. Lakini, ukweli unabaki miongoni mwa wapigania uhuru wa Tanganyika kuwa ndiye aliyemkaribisha Baba wa Taifa, Julius Nyerere kulala nyumbani kwake na kupanga mikakati ya kusaka uhuru.

Ndiye mzalendo ambaye kwa heshima yake, leo anaenziwa katika Uwanja wa Soka uliopo mjini Mtwara kupewa jina lake la Nangwanda Sijaona.

Itakumbukwa kuwa mwaka 1955, Nyerere alitembelea jimbo la Kusini na kufika Newala nyumbani kwa Sijaona, alikolala wakashirikiana kupanga mipango ya kuikomboa Tanganyika.

Ni mwaka huo ambao Sijaona alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa TANU wilayani Newala, kisha mwaka mmoja baadaye, akachaguliwa Mwenyekiti wa TANU jimbo la Kusini, ndipo akalazimika kuhamia Lindi kulikokuwa makao makuu ya jimbo.

Kuchaguliwa kwake kushika nafasi hizo, kulitokana na umahiri na ujasiri wa kuunga mkono kazi ya kupigania uhuru wa Tanganyika, hata akaamua kuacha kazi serikalini, kujiunga na TANU.

Mpigania uhuru huyo alifariki Januari 28, 2005, kama angekuwa hai, angekuwa na miaka 96, ameacha historia ya kulifanyia taifa mambo makubwa.

Anapotajwa kisiasa, ndiye miongoni mwa waasisi wa vyama vya siasa vya ukombozi akianzisha Tanganyika African Association (TAA), baadaye TANU na hatimaye CCM.

Mzizi wa nyota ya uongozi wake, ulianza kung'aa masomoni Minaki, aliposoma sekondari, ikielezwa kuwa alikuwa na nidhamu na unadhifu mkubwa , hapo aliteuliwa kuwa msaidizi wa kiranja mkuu akisimamia chakula.

Pamoja na jukumu hilo alikuwa mwandishi wa makala, barua nyingi, hata majarida na magazeti yanayohusu mambo ya siasa, licha ya kupigwa marufuku na serikali ya kikoloni.

Baadaye mwaka 1952, alipomaliza kidato cha sita, alianza kazi ya uandishi wa habari Ofisi ya Sekretari Mkuu, Idara ya Uhusiano wa Umma, akiwa mhariri wa gazeti la kila siku la 'Habari za Leo.'

Ni kazi aliyofanya kwa miaka miwili hadi 1954, alipoacha na kwenda kuwa Mtendaji Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya Newala, kwa muda wa mwaka mmoja.

Sijaona aliyezaliwa Novemba 24, 1928, kijijini Mnyambe wilayani Newala mkoani Mtwara, katika familia ya wazazi wakulima alipata elimu katika shule ya Msingi Utende kuanzia mwaka 1937.

Baada ya hapo, akahitimu darasa la nne mwaka 1942 akikofaulu na kuendelea na masomo ya darasa la tano hadi la nane, akiwa katika Chuo cha Mtakatifu Joseph, kilichoko Chidya Masasi.


Lawi Nangwanda Sijaona. **PICHA: MTANDAO**

Safari yake ya masomo ngazi ya juu sekondari, kidato cha tatu hadi sita alikuwa katika shule ya Mtakatifu Andrea, Minaki, Kisarawe mkoani Pwani, alikohitimu mwaka 1951. Baadaye akajiunga na Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda kwa masomo ya juu chuoni.

**HARAKATI ZAIDI**

Licha ya kufanya kazi serikalini, Sijaona alijiunga na siasa za TAA, akipewa kadi namba 204. Kikubwa kinachotajwa kuvuta upenzi wake ni haki za kitaifa kwa wananchi wenzake, hatua aliyofanya kwa siri.

Ikumbukwe serikali ya kikoloni wakati huo, iliwazuia watumishi wake kujiingiza kwenye siasa, lakini akaifanya kwa siri, ikiwamo kumkaribisha Mwalimu Nyerere, aliyekuwa akianza harakati za ukombozi.

Historia yake zaidi inaonesha, mwanasiasa huyo aliishi Lindi akifanya kazi za TANU bila malipo, vilevile akishika wadhifa wa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya TANU, baadaye katika harakati hizo alienda kikazi India.

Inaelezwa, wakati wa kurejea nyumbani ndege ilitua katika uwanja wa Nairobi, Kenya, akashikiliwa kwa saa tatu na askari kanzu wa wakoloni, ingawa kosa lake halikuelezwa.

Kilikuwa kipindi India ilipata Uhuru Agosti 1947, kisha ikaunga mkono nchi nyingi za Kiafrika kusaka uhuru, ikiwamo kutoa nafasi nyingi za kielimu kwa Waafrika wakasome, ili wawe na utashi na uwezo wa kujikomboa. Tanzania, mnufaika mmojawapo ni Waziri Mkuu mstaafu John Malecela.

Mwaka 1958 harakati za siasa za TANU kuikomboa Tanganyika zikipamba moto, ulifanyika uchaguzi wa kwanza wa serikali za mitaa na mkongwe Sijaona, akajitosa na kuchaguliwa diwani, pia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Lindi.

Ni ushindi uliomfanya kuweka historia kwa kuwa Mwenyekiti wa Kwanza Mwafrika wa Halmashauri za Miji Afrika Mashariki.

Aidha, nyota yake ilizidi kuwaka, mwaka 1959 kwenye Uchaguzi wa Kura Tatu (ulihusu Mzungu, Mhindi na Mwafrika), Sijaona aliteuliwa na TANU kuwakilisha jimbo la Kusini, alikochaguliwa bila kupingwa.

Haikuchukua muda mrefu, mwaka 1960 akachaguliwa mbunge wa Wilaya ya Lindi.

INAENDELEA UK.13

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Kinachohitajika ni kurejesha rasilimali kwa Watanzania

WATANZANIA wanaposherehekea miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika uliopatikana Desemba 9, 1961, mwanaharakati Gemma Akilimali, anaona kuwa licha ya miongo sita ya kujitawala, rasilimali za taifa hazijawanufaisha wananchi kikamilifu na kuleta maendeleo ipasavyo.

Anaona maliasili kama madini kuanzia almasi, tanzanite, bahari na misitu hazijarejeshwa kwa Watanzania na kuwanufaisha kama ambavyo uhuru ulitarajia.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, anasema lengo la uhuru lilikuwa kumuondoa mkoloni aliyetumia rasilimali za taifa kuendeleza unyonyaji na kujitawala ili kuzitumia kuwanufaisha wananchi.

Mwanaharakati huyu wa usawa wa kijinsia, mpinzani wa mfumo dume na mtetezi wa ajenda ya kurudisha rasilimali kwa wananchi, anaeleza zaidi...

**SWALI: Ni kitu gani unatamani kuona kingefanikiwa kikamilifu kama ambavyo uhuru ulikuwa umekusudia kwenye eneo la rasilimali?**

**JIBU:** Tulipopata uhuru tulikuwa na maadui wakuu watatu ujinga, umaskini na maradhi, ambao hadi leo tunakabiliana nao.

Ujinga, ni changamoto bado ipo licha ya jitihada nyingi kufanyika , wapo wanaomaliza shule bila kujua kusoma, kuandika wala kuhesabu.

Lakini eneo jingine ninalotaka kulizungumzia ni ukweli kuwa hatujaweza kuwa na elimu ya kung'amua mbinu mbalimbali za kutumia utajiri wa rasilimali zetu kubadilisha maisha yetu.

Mfano madini tuliyonayo, kuyachakata na kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotoa ajira, kuuzwa nje kupata kodi na uwekezaji kwa watu wetu badala ya kusubiri kampuni za kigeni.

Tunazungumzia wawekezaji karibu kila sekta waje wawekeze kwenye kilimo, utalii na madini.

Ukiangalia kwa miaka yote hii hatuna zana za kilimo tunazotumia mfano mbolea haipatikani, wakulima wetu wanategemea mvua na pale tunapotaka kuwa na mradi wa kilimo lazima kutafuta wawekezaji wa kigeni.

Hata pale tunapowatafuta kama taifa tunanufaikaje na rasilimali zetu hizo?

Inavyoonekana manufaa hayajawa ya kuridhisha kwenye rasilimali zetu na kwenye uwekezaji na ubinafsishaji, ndiyo maana rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, anasema katika kitabu chake kuwa moja ya yaliyomnyima usingizi ni ubinafsishaji ambao haukuridhisha.



Miradi mikubwa wa Liganga na Mchuchuma mkoani Njombe inalenga kuchimba makaa yam awe pamoja na chuma kuzalisha nishati na bidhaa za vyuma. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Tulitakiwa tugutuke na kuona kuwa kutoa rasilimali zetu kila wakati ziendelezwe na wageni na sasa tutegemee kupata faida kupitia kazi yao kunatuachia changamoto nyingi zaidi.



Mwanaharakati Gemma Akilimali

Tulitakiwa tugutuke na kuona kuwa kutoa rasilimali zetu kila wakati ziendelezwe na wageni na sasa tutegemee kupata faida kupitia kazi yao kunatuachia changamoto nyingi zaidi.

Ni sawa tunahitaji utaalamu na teknolojia lakini si kwa kuachia rasilimali zitwaliwe, zimilikiwe na kuendeshwa na wageni nashauri tuajiri wageni na wataalamu lakini si kuwaachia rasilimali zetu kwa jina la kuwekeza na wao wafanye kama wanavyotaka tukiamini kuwa tunafaidika, naona hili lina walakini.

Ninatamani kuona wachumi, wahandisi, wapanga mipango, wanasayansi wetu wakituongoza kwenye uwekezaji siyo wageni hao kukabidhiwa rasilimali pamoja na ardhi.

**SWALI: Kuna maeneo ambayo watu wamepata kazi, kumekuwa na mabadiliko ndani ya jamii hilo nalo unalizungumziaje?**

**JIBU:** Utajiri wa Tanzania ni mkubwa kuanzia madini, bahari, utalii, ardhi na misitu hivyo na vinginevyo vingetosha kuendeleza sekta ya elimu, afya na maji bure lakini hata sasa sekta hizo muhimu hazijaweza kunufaisha wananchi kikamilifu.

Tiba ya watoto kupitia toto afya kadi, ilikwama na sasa imerejeshwa. Wazee bado hawapati huduma za kimatibabu. Udumavu unatajwa kuongezeka ni zaidi ya asilimia 30, utapiamlo bado ni tatizo, miundombinu yetu hairidhishi na maji safi na salama ni changamoto mijini na vijijini.

Suala la uwekezaji tukiliangalia tunaona kuwa kuna migogoro ya ardhi, vilio kwenye mashirika yetu na wachimbaji madini wadogo wanalalamikia wawekezaji wamechukua rasilimali na wananchi hawajabaki na kitu, au hata kama ni fidia ni kiduchu na wamebaki na changamoto zaidi.

Tunaporuhusu rasilimali kuendelea kuchukuliwa tena kwa ridhaa yetu, tofauti na ilivyokuwa kabla ya uhuru wakoloni wakijichukulia wanavyotaka hatujafikia kile au matarajio ya uhuru wetu.

Tukumbuke kabla ya uhuru mipango ya kumiliki, uwezekaji na kuvuna rasilimali ilipangwa na wakoloni zama hizi linapaswa liwe jukumu letu wenyewe.

Hata kama tutasema wapo walionufaika na taifa linapata faida kwenye madini, utalii na ubinafsishaji wa mashirika na viwanda ni wachache si jambo la kupiga kifua na kujivunia baada ya miaka 63 ya uhuru.

**SWALI: Wanaharakati mna mchango wenu kuhamasisha mabadiliko, kufikia matamanio ya uhuru unadhani mmefanyakazi vya kutosha?**

**JIBU:** Tunafanya juhudi lakini wakati mwingine tunaonekana wapinzani, lakini tunajiuliza ina maana kuwa hakuna yeyote serikalini aliyeuona ukweli kwenye ushauri na harakati zetu? Viongozi hawayaoni matatizo ya wananchi wetu kwa kusikiliza tunayoyazungumzia?

**SWALI: Kauli mbiu ya uhuru ni 'uhuru na kazi', taifa limeweza kuisimama hadi sasa?**

**JIBU:** Vijana wetu hawafanyikazi na walio wengi wanataka kupata mali na mafanikio ya kuchumi kwa njia za kidanganyifu.

Watoto wetu hawataki kufanyakazi, zamani elimu ililenga kujitegemea na ilifundishwa shuleni wanafunzi wakafahamu kilimo, ufugaji na uzalishaji lakini sivyo.

Elimu hiyo imeondolewa wanamaliza shule hawafahamu mbinu zozote za kilimo, ufundi na uzalishaji kwa jumla tena hawawezi kujitegemea wala si wapenzi wa kufanyakazi.

Ni lazima tuwahimize zaidi vijana wetu kufanyakazi kwa bidii kwa sababu inavyoelekea wengi hawazalishi.

Maendeleo siyo kukaa vijweni na kukwepa kazi lakini kutafuta fedha na mfanikio kwa mbinu za kidanganyifu na kihalifu. Wajue kuwa hawawezi kufikia mafanikio ambayo taifa liliyatamani wakati wa kupigania uhuru kama hawatafanyakazi kwa bidii, maarifa na juhudi.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Tanzania iinuke kufikia miaka 100 ya uhuru iking'ara zaidi

NI hongera kwa taifa kutimiza miaka 63 ya uhuru ikiwa imebakia miongo michache kufikia jubilii ya miaka 100 ya uhuru wa Tanganyika, itakayosherehekewa Desemba 9, mwaka 2061.


Sherehe za uhuru jana hazikuadhimishwa kitaifa, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa maelekezo ya kusherehekea ngazi za mikoa. Amefuta maadhimisho ya sherehe za miaka 63 ya uhuru kitaifa na kuelekeza zifanyike katika ngazi ya mikoa, kwa kutoa huduma za kijamii, kupanda miti , usafi wa mazingira, masoko, hospitalini, kambi za wazee na wenye mahitaji maalum.

Wakati Watanzania wanasherehekea kumpinga na kumshinda mkoloni, yapo mambo ambayo raia wanayachukulia kawaida au poa, japo wanapaswa kuyabeba kama sababu kwa kila Mtanzania kusherehekea miongo sita ya mafanikio ya kihistoria.

Ikumbukwe wakati mataifa mengine ya Kiafrika yalipopata uhuru yalijitumbukiza kwenye vita, machafuko na migogoro, Tanzania iliendelea kujiimarisha kiuchumi kadhalika kuwa nchi ya amani na kubaki kwenye misingi bila kuvurugana.

Zipo nchi baada ya uhuru ziliingia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe, lakini Tanzania iliendelea kuwa kimbilio la wanaoteseka, chemchemi na kisiwa cha amani, utulivu na maridhiano na hilo ni jambo la kujivunia zaidi.

Inawezekana Tanzania imeendelea kuwa na utajiri mwingi zaidi kuanzia madini, ardhi, mifugo na vivutia watalii katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.



Mwalimu Nyerere alipowasha Mwenge wa Uhuru 1961.
**PICHA: MTANDAO**

Haya yote ni mambo bora na ya kusherehekea kwa sauti kubwa na shangwe nyingi.

Lakini ikiwa miaka 63 iliyopita imekuwa ya kushikilia na kudumisha amani na utulivu, kujenga uchumi, maridhiano na kuachana na mafarakano, miaka 37 ijayo ili kufika miaka 100 lazima iwe ya kufikia maendeleo endelevu kwa kila sekta.

Ni kwa kurejea zile taarifa kuwa nchi za Asia kama Korea Kusini na China zilikuwa kwenye kiwango kimoja cha kiuchumi miaka ya 1960 lakini leo ziko mbali na ndizo injini za uchumi duniani.

Licha ya kwamba mataifa hayo yalikuwa pamoja na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania 1960, miongo mitatu au miaka 30 baadaye yaani kuanzia 1990 zilizizidi kwa kishindo nchi za Kiafrika.

Miaka 63 iliyopita ni uthibitisho kwamba watu wamesimama kulinda umoja na utaifa wa Tanzania na Zanzibar.

Licha ya kuwa na makabila zaidi ya 130 taifa limebakia kuwa moja na hilo ni jambo la kujivunia lakini sasa likereketwe kufikia maendeleo na kuuaga umaskini.

Japo Watanzania Bara na Zanzibar ni wengi hakuna wazo la kutengana na kila siku ni lazima kuimarisha na kudumisha umoja wa kitaifa na mshikamano. Watanzania wameelewa kuwa pamoja na changamoto, kupanda na kushuka milima na mabonde 'Tanzania is there to stay' na kwamba lazima kuendelea kuiboresha na kuijenga zaidi kila uchao.

Sasa ni wakati wa kufikiria ni wapi Watanzania wanataka kwenda na wanafikaje? Cha msingi ni uongozi uendelee kuwa thabiti na wenye maono makubwa.

Watanzania wameimarika tangu uhuru licha ya kushindwa kufikia ilipo Korea Kusini au China sasa, lakini ili waweze kuruka masafa mengine wanahitaji uongozi bora zaidi na zaidi wenye maoni mapana yakuifikisha miaka 100 ikiwa bora zaidi.

Wananchi na vongozi lazima watambue kuwa bado ni nchi ya watu wengi maskini na wasio na elimu bora ambao pato la mtu mmoja mmoja ni takriban Sh 3,000,000 (dola 1,200) kwa mujibu wa Benki ya Dunia, kwa mwaka.

Lakini huo ni wastani wa kitakwimu, wengi wanaishi chini ya dola moja (Shilingi 2,600), kwa kiwango hicho ya shilingi kwa siku. Ili kufaulu miaka 37ijayo sera zinazopitishwa lazima ziakisi vipaumbele, hasa ukweli kwamba bado taifa halijaweza kuwezesha raia kupata chakula au milo mitatu, kutibu, kusomesha kutoa huduma muhimu kwa gharama rafiki.

Changamoto kwa viongozi na utawala wa awamu zote za sasa na zijazo iwe ni kuona uchungu kuwa watu bado ni maskini, wanaoishi kwenye vibanda vya nyasi, makuti na matope au matembe.

Uongozi usikubali kuwapo na kiwango cha juu cha vifo vya watoto wachanga kwa kiasi cha watoto 43 kwa kila 1,000 wanaozaliwa hai.

Viongozi waone uchungu wakijipiga vifua na kujiambia kuwa ni aibu kuona wanawake wetu wanakufa kwenye uzazi yaani roho za wazazi 104 kati ya 100,000 zinapotea kutokana na masuala ya uzazi.

Iwakere viongozi kuona kuwa wasichana wanapewa mimba na kuozwa utotoni, watoto wanakatiliwa kwa kiwango kikubwa wakiingiliwa kinyume na maumbile na kujansiwa na hayoyote ni kutokana na umaskini kisha kulitokomeza tatizo hilo.

Si suala la siasa au ni nani anayeongoza. Ni wajibu wa viongozi kuwapa watu mambo muhimu wanayohitaji ili kuishi maisha ya furaha hasa kuwa na afya na bora, elimu, maji safi, makazi bora na bila kulia upungufu au ukosefu wa chakula.

Tanzania inapoisogelea miaka 100 ya uhuru wa Tanganyika Watanzania wasionekane tena wakipokea bidhaa muhimu kama 'taulo za kike' kutoka kwa wahisani.

Haipendezi taifa likipokea misaada kama kujengewa vyoo shuleni , kuwekewa maji na wafadhili wa mataifa wahisani badala ya serikali kuweka huduma hizo.

Ufike wakati kama taifa kujihusisha kikamilifu na rasilimali za taifa na kuzitunza. Kadhalika kutunza fedha za umma, kuacha ufisadi na ubadhirifu ili kuwa a watu wenye afya tele wanaosherehekea maiaka 100 ya uhuru na ushindi.

# Mpigania uhuru aliyemkaribisha Mwalimu Nyerere kwenye vyama

**INATOKA UK.11**

Katika uchaguzi wa mwaka 1965, Sijaona alirudi kwao Newala kuwania ubunge na kushinda kwa kishindo, ilipofika 1970, awania tena nafasi hiyo, akashinda bila kupingwa katika jimbo hilo.

**UONGOZI SERIKALINI**

Mwaka 1961 baada ya Uhuru , aliteuliwa Naibu Waziri Serikali za Mitaa na Tawala za Majimbo na 1962, alikahamishwa kuwa Wizara ya Fedha, baadaye Waziri wa Mila za Taifa na Uongozi wa Vijana.

Ilipofika mwaka 1964 wakati wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, akawa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais.

Umahiri kikazini ulimfanya ahamishwe katika wizara mbalimbali, zikiwamo Ardhi, Maji na Makazi; Mambo ya Ndani ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais na Afya na Ustawi wa Jamii.

Mwaka 1972, serikali ilipofuta Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuanzisha mfumo wa Madaraka Mikoani (iliyodumu hadi 1982), ukilenga kupeleka mamlaka za serikali ngazi za msingi kuanzia mkoa mpaka vijiji, Sijaona akawa Mkuu wa Mkoa wa Ziwa Magharibi (sasa Kagera), akiongoza kwa miezi sita.

Ndani ya kipindi hicho, Sijaona akapelekwa mkoa wa Mwanza, alikodumu hadi mwaka 1976, akahamishiwa kwa nafasi hiyo kuongoza mkoa wa Kilimanjaro hadi 1980, akahamishiwa kwa kazi hiyo mkoani Mtwara.

Ilipofika 1983, akiwa na miaka 55 aliomba kustaafu, hata akarejea maisha ya ukulima, lakini kwa uwezo wake wa uongozi, aliteuliwa mbunge hadi lilipovunjwa mwaka 1985.

**NDANI YA CHAMA**

Historia inaonyesha kuwa mwaka 1956 aliiwakilisha TANU katika mkutano wa Asian Socialist Conference, uliofanyika Bombay nchini India.

1959 akawa Mjumbe wa Kamati Kuu ya TANU, pia Katibu Mkuu wa kwanza wa Umoja wa Vijana wa TANU, kadhalika, mjumbe wa Tume ya Kuangalia Muundo wa Serikali ya Tanganyika, baada ya uhuru.

Baadaye mwaka 1961, akateuliwa kuwa mjumbe wa Mkutano wa Katiba, ilipofika 1962 wakati huo akiwa Naibu Waziri wa Fedha, alikuwa Mwakilishi wa Serikali ya Tanganyika katika Kamati ya Nchi 11 ya Kiuchumi, Afrika.

Inaelezwa kwamba alikuwa na jukumu la kushauriana na serikali za Afrika kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mwaka 1976, Sijaona alichaguliwa kuwa mjumbe wa Tume ya Watu 20 iliyoandaa katiba ya CCM, iliyoteuliwa na Rais Nyerere, kuandaa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## KUMBUKIZI ZA MASUALA YA UHURU



Gavana wa mwisho wa Tanganyika Edward-Twinning,



Mwalimu Nyerere akiwa na baadhi ya viongozi wa serikali akiwamo Waziri Mkuu Rashid Kawawa (wapili kulia), Job Lusinde (kulia)



Mwalimu Nyerere pamoja na viongozi wa Afrika wakiwa Chuo Kikuu cha Makerere Uganda kuimarisha elimu baada ya uhuru wa mataifa ya Afrika Mashariki. **PICHA: MTANDAO**




Makumbusho ya Baba wa Taifa Julius Nyerere yaliko nyumbani kwake kijijini Butiama



MWalimu Nyerere akitafuta ushirikiano wa kimataifa pamoja naye ni Rais wa zamani wa Marekani, John Kennedy.



# Watu wenye ulemavu wapewa msaada cherehani

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Sightsavers kupitia mradi wa uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu limetoa misaada mbalimbali ikiwamo cherehani kwa watu hao Manispaa ya Singida na Wilaya ya Mkalama ili wajikwamue kiuchumi.

Mratibu wa Uwezeshaji Kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Singida, Upendo Minja akizungumza kuhusu msaada huo mwishoni mwa wiki, alisema wamepatiwa baada ya kupewa mafunzo ya ujasiriamali.

"Tumetoa vifaa visaidizi kwa watu wenye ulemavu, mitungi ya gesi, cherehani, baiskeli, mashine ya kufumia masweta na bidhaa za dukani ambazo ni sukari, soda na sabuni ili wavitumie kujikwamua kiuchumi," alisema.

Aliongeza kuwa: "Kundi la walemavu linaonekana kama ni la watu wanaohitaji msaada tu lakini kimsingi ni kundi ambalo linajiweza na wengi wanamiradi yao ya biashara, tunaomba watu wengine wajitokeze kusaidia jamii hii."

Naye, Katibu wa Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS) Mkoa wa Singida, Nassoro Ernest, alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo mkubwa kwa walemavu na kuomba jamii kuendelea kutoa misaada inayosaidia wajikwamue kiuchumi na kuondokana na utegemezi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Shila Mwashiuya, alitoa wito kwa wananchi kuwasaidia watu wenye ulemavu wanapokwenda kuomba msaada na siyo kudhihakiwa kwa kuwa hawajapenda kuwa walemavu.

"Mlemavu akija kukuomba msaada msaidie maana hatujui leo mzima kesho hujui utakuwa mlemavu, sisi sote hapa ni walemavu watarajia," alisema.

Dk.Mwashiuya aliwataka wanufaika wa misaada hiyo waitumie vizuri ili kuleta chachu kwa wadau wengine waweze kuleta misaada zaidi.

# Polisi: Uchukuaji, utunzaji, sampuli uzingatie weledi

**Na Idda Mushi,** DODOMA

OFISA Mnadhimu wa Kamisheni ya Kisayansi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Theopista Mallya amesema lazima uchukuaji, utunzaji, usafirishaji na uchakataji wa sampuli za makosa ya jinai uzingatie weledi ili haki itendeke kwenye maamuzi ya kisheria.

Mallya aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha wadau wa sayansi jinai kilichowakutanisha wataalamu wa Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) Kanda ya Kati kwa ajili ya kujadili usimamizi wa sampuli.

Alisema ni muhimu wadau hao ambao wako kwenye mlolongo wa haki jinai wafanye kazi zao kwa umakini, usahihi, ushirikiano na kutegemeana.

"Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai na sheria ya vinasaba vya binadamu zinatoa mamlaka kwa wataalamu wa afya na maafisa wa Jeshi la Polisi kuchukua na kuwasilisha sampuli mbalimbali kwenye maabara ya Mkemia Mkuu kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara na kutumiwa kama kielekezo kwa hatua mbalimbali za maamuzi ya kisheria," alisema.

Alisema polisi, madaktari na wadau wengine muhimu wakijengewa uwezo wa kufanya kazi yao kwa weledi na kufuata taratibu za kiuchunguzi watatoa matokeo ambayo hayataleta shaka yeyote katika maamuzi.

Naye, Meneja wa Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati Dodoma, Gerald Meliyo Mollel alisema uchukuaji wa sampuli ukikosewa sio rahisi kupata majibu sahihi hivyo watuhumiwa na walalamikaji hawatapata haki stahiki.

Alieleza kuwa nia ya kuwakutanisha wadau hao ni kuwafundisha namna bora ya uchukuaji, uhifadhi, usafirishaji na uchakati wa sampuli mbalimbali za jinai ili haki itendeke mahakamani.

Mmoja wa washiriki ambaye ni Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Dodoma kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Paschal Marungu alipongeza elimu hiyo na kwamba itaongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

"Unajua siku hizi kuna ongezeko kubwa la makosa ya mauaji, ubakaji, ulawiti, yote haya ili kuthibitisha ushahidi usio na shaka mahakamani...elimu hii itatusaidia sana tunapokea ratibu upelelezi jalada likijaa ofisini, kwa kuwa na upelelezi uliokamilika, ushahidi mwingi umekuwa unakwama kwasababu ya kukosa ushahidi wa kitaalamu,"alisema.

Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa, Timothy Lyon, aliwaasa wapelelezi kuwa makini katika upelelezi wao ili kesi zao ziwe na mafanikio mahakamani.




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego,akipanda mti jana katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa huo wakati wa maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Kabla ya zoezi la kupanda miti Mkuu wa Mkoa alitembelea wodi za hospitali hiyo na kutoa zawadi mbalimbali kwa wagonjwa. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kuboreshwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji imesema imejipanga kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji hapa nchini, ili kuhakikisha wakulima wanalima zaidi ya mara mbili ndani ya msimu wa kilimo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji Miundombinu wa Tume hiyo, Mwinyijuma Tengeneza alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumzia kuhusu kukamilika kwa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Membe wilayani Chamwino.

Alibainisha kuwa lengo la kuboresha miundombinu hiyo ni kuwasaidia wakulima waitumie kujikwamua kiuchumi.

Tengeneza alisema moja ya miundombinu inayoendelea kuboreshwa ni ujenzi wa bwawa la kilimo cha umwagiliaji la Membe ambalo litakuwa likivuna maji kutoka mikoa ya Manyara na Singida na yatawasaidia wakulima kuendesha kilimo cha umwagiliaji.

"Bwawa hili lina faida kubwa sana kwa wakulima kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa sababu lina uwezo wa kuhifadhi maji mengi ambayo yatavunwa kutoka mikoa iliotajwa,"alisema Tengeneza.

Alisema mradi wa ujenzi wa bwawa hilo wenye thamani ya Sh. bilioni 12, unatarajia kukamilika mwakani na litaongeza ushawishi kwa jamii kufanya kilimo cha umwagiliaji.

Tengeneza alisema dhamira kubwa ya serikali ni kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo cha umwagiliaji, ndio maana imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya kilimo ili kuhakikisha wakulima wanainuka kiuchumi.

Aidha, alisema katika uwekezaji uliofanywa na serikali tume hiyo imefanikisha kununua mitambo 48 ambayo inafanya kazi ya uboreshwaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali hususani katika mradi wa BBT na miradi mingine inayotekelezwa na serikali.

Aidha, alisema kuwa uwapo wa mitambo hiyo unasaidia uchimbaji wa mabwawa pamoja na visima ili kupanua na kuongeza wigo wa kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima.

Hata hivyo alisema kutokana na uwekezaji uliofanywa na serikali, umechangia kushawishi sekta binafsi kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kuongeza kuwa tume hiyo imekuwa ikishirikiana nao kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinakua.

Naye, Mkulima Lameck Chipego alisema ujenzi wa bwawa hilo ukikamilika utawanufaisha wakulima wengi wanaofanya kilimo cha umwagiliaji.

Alisema wanaishukuru serikali kutokana na uwekezaji inayofanya kwenye sekta ya kilimo kitendo kinachozidi kushawishi jamii hususani vijana kujikita katika kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Hivyo, aliwaasa wakulima kujikita kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji ambacho kitatoa faida kubwa.



# SMZ kushirikiana na sekta binafsi kusogeza nishati kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwenye sekta mbalimbali ikiwemo ya nishati ili kusogeza huduma kwa wananchi na kukuza uchumi.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaib Hassan Kaduara alisema hayo juzi visiwani Zanzibar wakati akizindua kituo cha kwanza cha mafuta cha Puma Energy Tanzania, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Zanzibar katika kukuza uwekezaji.

Waziri Kaduara alisema anatambua mchango wa kampuni hiyo katika kuunga mkono maono ya serikali kuhusu suluhisho endelevu na jumuishi la huduma za nishati.

Alisema mchango wa kampuni hiyo pia umeimarisha sekta ya nishati na kuwa mdau muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

Waziri Kaduara alisema serikali inaipongeza kampuni hiyo kwa mchango wake thabiti katika sekta ya anga ya Zanzibar, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa sekta yao ya utalii ambayo ni msingi wa uchumi wa Zanzibar.

"Jitihada zenu zimepelekea wasafiri kutoka maeneo mbalimbali kutembelea visiwa vyetu vizuri bila ya changamoto zozote na kusaidia kuimarisha na kuitangaza sifa ya Zanzibar kama kivutio cha kitalii chenye hadhi ya kimataifa," alisema.

Alisema mbali ya sekta ya mafuta kampuni hiyo imekuwa ikishiriki katika kuchagiza maendeleo ya wananchi akitoa mfano wa kujenga matundu ya choo ya ziada na kufanya maboresha ya miundombinu ya Shule ya Kisiwandui na kuwanufaisha wanafunzi zaidi ya 2000.

Amesema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa kampuni hiyo, kwamba dhamira yao ni muhimu katika kuijenga Zanzibar yenye ustawi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah alisema kuzinduliwa kwa kituo hicho cha kwanza na kipya cha mafuta na huduma za ziada Zanzibar ni ishara ya kujizatiti kwao katika kuziwezesha jamii, kutoa huduma zenye ubora na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

Alisema: "Kwetu ni siku muhimu kwa mara ya kwanza tunafungua kituo cha kwanza Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kuendelea kusambaza huduma za upatikanaji wa mafuta na nyinginezo kwenye soko la Zanzibar".

Alisema Puma Energy Tanzania iliingia katika soko la Zanzibar mwaka 1994 ikiwa inafahamika kama BP Tanzania hadi mwaka 2011 Puma Energy Tanzania iliponunua hisa za BP.

Alisema wamekuwa wakishiriki katika ukarabati wa vyumba vya madarasa na ujenzi wa vyoo vipya katika Shule ya Kiswandui na wiki iliyopo walishiriki katika wiki ya nenda kwa usalama barabarani.

Hata hivyo alisema Puma Energy Tanzania kwa Zanzibar inaenda mbele zaidi ya kutoa huduma za mafuta, inahusisha pamoja na kujenga ushirikiano, kutengeneza fursa na kuwezesha maisha ya jamii wanazozihudumia.

Alisema ajenda yao ni kuhakikisha Zanzibar inakuwa na suluhisho la huduma za nishati za kiwango cha kimataifa.

Fatma alisema katika kuchangia katika ajira za ndani, wamekuwa wakiunga mkono Zanzibar kupitia shughuli za mafuta ya anga na kutoa ombi kwa Serikali ya Zanzibar kusaidia upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji wa nishati ya mafuta ya magari na anga.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Puma Energy Tanzania, Dk. Selemani Majige alisema wanatambua upatikanaji wa huduma za nishati ni msingi wa maendeleo ya kiuchumi na dhamira yao ni kutoa mchango muhimu katika kuleta mabadiliko Tanzania.

Dk. Majige alisema Puma Energy Tanzania inajivunia kushirikiana na serikali ambayo inamiliki asilimia 50 ya hisa za kampuni.

Alisema ushirikiano huo unasisitiza dhamira yao ya pamoja ya kuendeleza sekta ya nishati na kukuza ukuaji endelevu kwa manufaa ya Watanzania.




Wakusanya ushuru kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho Dar es Salaam wakisubiri makondakta wawape pesa za ushuru jana. Hata hivyo, wanalalamikiwa na abiria kuwa wanachelewesha daladala kuondoka kituoni hapo kwa utaratibu wao wa kusubiri madereva watoke kituoni na kuwasimamisha walipe ushuru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mvua ya upepo yaezua nyumba 13 Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MVUA iliyoambatana na upepo mkali imeezua nyumba 13 na zingine kadhaa kuta kudondoka katika Kata ya Mlowa Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani Njombe.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki ambapo mitaa iliyoathiriwa na mvua hizo ni Mkolango ambapo nyumba sita zimeezuliwa, Mludza (5), Itipingi (2) na Mgewalala nyumba moja.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Diwani wa Kata ya Mlowa, Odilo Fute alisema baadhi ya wananchi ambao nyumba zao zimedondoka wamehifadhiwa kwenye nyumba za majirani.

Fute alisema hakuna kifo wala majeruhi badala yake kumetokea uhalibifu ambao umetokea kwa kiasi kikubwa ambapo aliwaomba wadau kuwasaidia wananchi hao ili waweze kuendelea na maisha yao.

"Ili kukabiliana na tatizo hili tunawaomba wadau watusaidie ili kurudisha makazi ya wananchi kwa sababu wamekata tamaa kutokana na tukio hilo ambalo limewakuta," alisema Fute.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mkolango, Jailos Ngimbudzi alikiri kutokea kwa maaafa hayo na nyumba sita kuathiriwa katika mtaa wake na kueleza kuwa wiki ijayo kamati ya maafa ya itakaa ili kuona athari iliyojitokeza na namna ya kuwasaidia waathirika.

Nao baadhi ya waathirika na mvua hizo akiwemo, Shadrack Kilamlya aliomba wadau wa mbao, mabati na misumari ili nyumba zao ziweze kuezekwa.

"Kwa kweli yamenikuta maana mvua ilipokuwa inanyesha nilikuwa hapo hapo na ilikuwa mvua kubwa yenye upepo mkali na hivyo ikaezua nyumba," alisema Kilamlya.

Kamati ya Maafa ya Halmashauri ya Mji wa Makambako imetembelea waathirika hao na sasa inaendelea na tathimini ili kuona namna ya kuwasaidia.

# Watatu familia moja wafariki dunia kwa radi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU watatu wa familia moja Elia Mhagama (37), Eric Mhagama (13) pamoja na Amos Haule (21) wakazi wa Kijiji cha Mawengi wilayani Ludewa mkoani Njombe wamefariki dunia kwa kupigwa na radi wakati wakijikinga na mvua kwenye kibanda.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alithibitisha kutokea kwa tukio hilo Desemba 4 mwaka huu majira ya saa nane mchana katika Kitongoji cha Danida kijiji cha Mawengi wilayani Ludewa.

Banga alisema familia hiyo ilipigwa na radi wakiwa shambani baada ya mvua iliyoambatana na upepo kuanza wakiwa wamejikinga kwenye kibanda cha kuhifadhia mazao.

"Chanzo cha tukio hili ni mvua kubwa zilizombatana na radi ndizo zilizopelekea vifo vya hawa watu kwa sababu walikuwa wamejibanza kwenye kibanda cha kuhifadhia mazao huko shambani," alisema Kamanda Banga.

Alisema miili ya marehemu hao ilihifadhiwa katika Kituo cha Afya Mlangali na baada ya uchunguzi ilikabidhiwa kwa familia kwa ajili ya shughuli za mazishi.

Kamanda Banga alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari kipindi cha mvua kutojificha kwenye maeneo mabichi au kwenye miti badala yake kwenye nyumba ambazo zimejengwa kwa bati.

"Lakini hizi nyumba ambazo zimeezekwa kwa nyasi nazo zinaakisi radi na zinapitisha ile miale kwa hiyo tuchukue tahadhari kwa kukaa sehemu ambazo ni salama," alisema Banga.

Kamanda Banga alisema jeshi hilo linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya hadhara ambayo inaendeshwa na mapolisi kata mkoani humo.

Awali kwa mujibu wa manusura wa tukio hilo, Atu Luoga alisema walikuwa shambani wakilima na mume wake ambapo mvua ilianza kunyesha ndipo wakaona ni vyema wakajibanze kwenye kibanda.

Alisema: "Mdogo wangu pamoja na mwanangu waliingia ndani ya kibanda huku mimi na mume wangu tulijibanza kwa nje na ghafla ilipiga radi na kumuua mume wangu, mtoto na mdogo wangu na hivyo nikapiga yowe na kuomba msaada".

Mtendaji wa Kijiji cha Mawengi, Rogatus Mgaya alisema wananchi wanapaswa kuchukuwa taadhari kwa kutojificha kwenye maeneo ya wazi au miti pindi mvua zinaponyesha.

## Serikali: TBS inatafsiri kwa vitendo maono ya Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema hatua ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kupatiwa cheti cha umahiri wa kutoa huduma ya ithibati ubora wa bidhaa inadhihirisha jinsi shirika hilo lilivyotafsiri kwa vitendo maono na miongozo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Kauli hiyo ilitolewa na mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, kwenye hafla ya kukabidhiwa TBS cheti cha umahiri wa kutoa huduma ya ithibati ubora wa bidhaa.

Dk. Abdalllah aliongeza kuwa hatua hiyo inadhihirisha umma kuwa kauli ya Rais Samia ya kuwa sasa tuko tayari kuingia kwenye masoko ya kimataifa tukiwa na bidhaa bora, TBS imeweza kukamilisha ndoto hiyo.

Alifafanua kuwa serikali imedhamiria kujenga misingi shindani na endelevu ambayo haiwezi kupatikana kama bidhaa siyo bora.

Aliongeza kusema kuwa serikali itaendelea kuimarisha uhusiano na taasisi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kupata ufadhili katika kuendesha taasisi hizo za udhibiti ubora.

Alisema mafanikio hayo yanawapeleka katika hatua nyingine ya mafanikio ya uchumi wa nchi yetu, kwani Tanzania imeingia kwenye eneo huru la biashara Afrika, soko ambalo linahitaji sana bidhaa na huduma zilizo bora.

Aidha, aliwashukuru wazalishaji hasa walioingia kwenye mchakato huo, kwani bidhaa zilizoingia kwenye mchakato huo zimeweka wigo mpana wa ithibati mahiri kwa kuwapa ushirikiano wa hali ya juu, kuruhusu TBS kufanya ukaguzi na kuhakiki katika zile bidhaa zilizowahusisha wakaguzi wa SADCAS.

Mkurugenzi wa TBS, Dk. Ashura Katunzi, alisema maabara zote tisa za TBS zimeishathibitishwa mifumo na zina ithibati.

Alisema kutokana na kuimarika kwa uhuduma za shirika, mifumo yake ya udhibiti wa ubora imekuwa ikipokea maombi ya viwanda kutoka nje, ili kuweza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

# Wanaume umri miaka 40 waitwa kupima tezi dume

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wanaume hususani wenye umri wa miaka 40 kuendelea kujitokeza kufanya uchunguzi wa saratani ya tezi dume.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mazrui alisema licha ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika uhamasishaji wa uchunguzi wa maradhi yasiyoambukiza ikiwamo saratani bado kasi ya wanaume ni ndogo visiwani humo.

Alisema wengi wa wanaume wamekua na hofu na uwoga wa kufanya uchunguzi wa tezi dume kwasababu bado wanahofia kipimo cha zamani cha uchunguzi kilichokuwa kikitumika.

Alisema kipimo kinachotumika hivi sasa katika uchunguzi wa saratani ya tenzi dume ni vifaa vya kisasa ambapo hutolewa damu na ikafanyiwa uchunguzi.

Aidha, alisema kuwa ugonjwa huo ukiwahiwa matibabu mapema unatibika, hivyo ni vyema kujitokeza kufanya uchunguzi.

Alisema uchunguzi uliofanywa na wizara hiyo katika wilaya mbili za Magharibi A na Magharibi B Unguja, kwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume ambapo jumla ya watu 2,722.

Mazrui alisema kati ya idadi hiyo walichunguzwa kati ya hao wanawake 26 waligundulikana na athari za matatizo saratani ya matiti, 24 saratani ya shingo ya kizazi na wanaume 100 waligundulikana na viashiria vya tezi dume.

Alisema ugonjwa huo ukifikia katika hatua ya mwisho siyo rahisi kutibika na hupelekea kifo hivyo ni vyema jamii kuhamasishana katika kufanya uchunguzi wa ugonjwa huo.

Mazrui alisema pia wanaume wanajazana kasumba ya kwamba ukifanyiwa upasuaji wa tenzi dume nguvu za kiume zinaondoka jambo ambalo siyo kweli.

Alisema kasi ya wagonjwa wa maradhi yasiyoambukiza ikiwemo saratani ni kubwa visiwani humo, hivyo ni vyema wananchi kuchukua tahadhari katika kujikinga na maradhi hayo.

Alisema miongoni mwa tahadhari hizo ni kufanya mazoezi, kula mlo sahihi na kuepukana na viashiria vinavyochochea maradhi hayo ikiwemo matumizi ya vileo kama matumizi ya pombe, sigara, tumbaku.

Hata hivyo aliwataka wanawake kuacha kuweka na kufukiza manukato katika sehemu zao za siri ili kuepukana na saratani ya shingo ya kizazi.




Kamanda wa kikosi cha usalama barabarani Tanzania, DCP Ramadhan N'ganzi akizungumza na vyombo vya habari baada ya kuongoza operesheni ya ukaguzi wa magari mbalimbali na kutoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva na abiria mkoani Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uzalishaji wa mpunga Zanzibar waongezeka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema uzalishaji wa mpunga umeongezeka, hatua inayochochea ukuaji wa uchumi wa kilimo na uhakika wa chakula kwa wananchi wa Zanzibar.

Amesema uzalishaji umeongezeka kutoka tani 1.5 za mpunga hadi kufikia tani 5.5 kwa msimu mmoja.

Shaame alisema hatua hiyo inatokana na ushirikiano wa kimkakati ikiwamo kati ya ubalozi wa Marekani na Korea Kusini katika kufadhili miradi ya kilimo visiwani Zanzibar.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa kilimo endelevu huko Kibokwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Waziri Shamata alisema kuwa ufadhili huo utaimarisha uzalishaji wa mazao na kuboresha maisha ya wakulima wa Zanzibar kupitia teknolojia na mafunzo ya kisasa.

"Tunaamini kuwa ushirikiano huu utasaidia Zanzibar kufikia malengo yake ya maendeleo endelevu katika sekta ya kilimo na kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji kwa njia rafiki kwa mazingira," alisema Waziri Shamata.

Aliongeza kuwa mradi huo ni sehemu ya jitihada za serikali za kuimarisha umwagiliaji na kuongeza thamani ya mazao ili kukuza uchumi wa kilimo na kuwataka wakulima kuendelea kushirikiana na kutumia fursa zinazotokana na mradi huo ili kuongeza tija na ustawi wa sekta ya kilimo.

Naye Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania, Eunju Ahn, alisema kuwa mradi wa kilimo cha umwagiliaji visiwani Zanzibar, ulioanzishwa mwaka 2019, umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuinua sekta ya kilimo.

Alisema kuwa mradi huo ni sehemu ya jitihada za Korea Kusini kusaidia maendeleo ya kilimo endelevu kwa kushirikiana na vijiji mbalimbali, vikiwamo Kinyasini, Cheju, Kibokwa, Kilombero na Chaani.

Balozi Eunju Ahn alisisitiza dhamira ya Korea Kusini kuendelea kushirikiana na Serikali ya Zanzibar na mradi wa Feed the Future Tanzania yenye dhamira ya kuimarisha sekta binafsi na kilimo tija katika kuhakikisha kilimo kinakuwa msingi wa maendeleo endelevu.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle, alisema kuwa mradi huo umeleta mabadiliko chanya kwa wakulima, hasa wanawake na vijana, ambao wamekuwa walengwa wakuu wa mafunzo na msaada wa uzalishaji.

Alisema zaidi kuwa mradi huo umeimarisha uwezo wa wakulima kuzalisha chakula bora na cha kutosha, siyo tu kwa matumizi ya ndani ya Zanzibar na Tanzania, bali pia kwa nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Balozi Battle alisisitiza dhamira ya Marekani ya kuendelea kushirikiana na Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya kilimo kwa lengo la kujenga jamii yenye ustawi wa kiuchumi na kijamii.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mattar Zahor Masoud, aliahidi kuhakikisha miundombinu ya kilimo iliyoletwa kupitia mradi wa kilimo endelevu kwa ushirikiano wa Marekani na Korea Kusini inalindwa na kuwa salama kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao mkoani humo.

Aliongeza kuwa mabalozi wa Marekani na Korea Kusini wameweka msingi imara wa maendeleo kupitia uwekezaji katika sekta ya kilimo, hivyo ni jukumu la wakulima na viongozi wa kijamii kuhakikisha uwekezaji huo unadumu na kuwanufaisha vizazi vijavyo.

## Tanzania yakabiliwa uhaba wa marubani 152

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Salim Msangi, amesema wanakabiliwa na uhaba wa marubani 152, jambo ambalo lisipoangaliwa vizuri nafasi hizo zinaweza kuchukuliwa na wageni.

Msangi aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu marubani waliomaliza masomo yanayofadhiliwa na Mfuko wa Mafunzo wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA Training Fund) na maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga Duniani (ICAD).

Alisema marubani waliopo hivi sasa ni 603. Kati yao, wa ndani ni 344 na wa nje ya nchi ni 259. Uhitaji wa marubani nchini ni 755, hivyo kuwapo upungufu ni marubani 152.

Alisema si kwamba watanzania hawawezi kuingia katika sekta hiyo. Changamoto iko katika gharama za kusoma. Rubani mmoja masomo yake yanagharimu zaidi ya Sh. milioni 200 na anayesomea ufundi wa ndege atatakiwa kulipia Sh. milioni 100.

Msangi alisema wazazi wengi hukosa fedha hizo za kuwasomesha watoto wao katika maeneo hayo. Ndio sababu ya kuanzishwa TCAA Training Fund kwa lengo la kufadhili mafunzo ya urubani na uhandisi wa ndege.

Alisema ufadhili wa mafunzo hayo utasaidia watanzania kusomea fani hizo kwa kuwa mafunzo hayo ni ghali na ni wazazi wachache wanaoweza kuyamudu.

"Pia ilionekana kwenye soko la ajira, kuna upungufu wa watanzania kwenye kada hizo," alisema Mkurugenzi Mkuu Msangi.

Alisema kuwa awali mfuko uliwasomesha marubani wanne ambao kwa sasa wameajiriwa na mashirika mbalimbali, hivyo kwa ujumla mfuko hadi sasa umesomesha watanzania 23.

"Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mchakato wa mafunzo yao, marubani hao walikutana na changamoto ya kufungwa kwa chuo walikokuwa wanasoma Uganda kutokana na UVIKO-19. Chuo kilifungwa mara mbili kutokana na changamoto ya ugonjwa huo uliokumba dunia," alisema.

Msangi alisema changamoto hiyo ilisababisha kuchelewa kumaliza mafunzo hayo ambapo kwa sasa wamemaliza na mategemeo yao ni marubani hao kuingia sokoni na kuajiriwa katika kampuni za ndege ili kukidhi uhaba wa marubani wazalendo uliomo katika kada hiyo na kukuza sekta ya usafiri wa anga.

Msangi alisema katika kuadhimisha Wiki ya Usafiri wa Anga Duniani Tanzania imefanya vizuri katika usalama wa anga pamoja na maeneo mengine na kuzidi kuaminika kitaifa.

Alisema zimesimikwa rada nne na kuona anga lote la nchi na hakuna ndege ambayo itaingia nchini bila kuonekana katika mfumo.

Msangi alisema kuwa kabla ya rada hizo, walikuwa wanaona anga lote kwa asilimia 20, hivyo kwa sasa wameimarisha na usalama wa anga uko vizuri.

Alisema kumekuwa na ongezeko la kampuni nne za mafuta ya ndege zinazouza nishati hiyo nchini, hali iliyochochea mafuta kutokupanda kulingamishwa na awali kulipokuwa na kampuni moja inayotoa huduma ambayo ingesababisha gharama kupanda katika eneo hilo.



Wanachama wa shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo WAJIKI pamoja na wanafunzi, wakiwa katika maandamano ya shirika hilo, kwa ajili ya kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Mbezi Beach Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# EU: Ukatili wa kijinsia ni kizuizi cha maendeleo

**Na Julieth Mkireri**

BALOZI wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Christine Grau amesema ukatili dhidi ya wanawake na wasichana si tu ni ukiukwaji haki za binadamu bali pia ni kizuizi cha kudumu cha maendeleo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita mjini hapa wakati wa mdahalo ulioandaliwa na UN Women, ukilenga kujadili mambo mbalimbali katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili.

Christine alisema katika kuangazia umuhimu wa Mpango wa Tatu wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto pamoja na kufanyika kwa mambo mengi, bado kazi kubwa inahitajika kufanywa.

"Pamoja na jitihada zinazofanyika, tunaendelea kukumbushwa kwamba mapambano dhidi ya ukatili wa jinsia yanaendelea na yanahitaji ushirikiano, kujitolea na ubunifu.

"Hakuna mtu anayepaswa kukabiliwa na ukatili kwa sababu ya jinsia, umri au hali yake. Hatuwezi kufikia ukuaji endelevu na shirikishi ikiwa hatuchukui hatua jasiri za kukabiliana na ukatili wa jinsia," alisisitiza.

Alisema kwa upande wao kama washirika wa maendeleo nchini, wanazingatia nyanja kadhaa muhimu kuhakikisha wanazuia na kukabiliana na vitendo vya ukatili ili ahadi ya 2030 ya ulimwengu bila ukatili dhidi ya wanawake na wasichana isiwe ndogo, bali iwe na uhalisia.

Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Susan Ngongi alisema ukatili wa kijinsia bado ni tatizo linaloathiri afya, heshima, usalama na uhuru wa waathiriwa, jambo ambalo ni ukiukwaji wa haki za binadamu na kikwazo kikubwa cha kufikia usawa wa jinsia na maendeleo endelevu.

Alisema kuwa kwa Tanzania, theluthi moja ya wanawake na wasichana wenye umri wa zaidi ya miaka 15 wanaripotiwa kupata unyanyasaji kimwili, kingono, kihisia au kiuchumi.

Suzan alisema wanawake na watoto wenye ulemavu pia wanakabiliwa na vikwazo zaidi kutokana na ubaguzi wa kijamii, upatikanaji mdogo wa huduma za usaidizi na ubaguzi wa kimfumo, hali ambayo inaendeleza tatizo la kibinafsi ambalo ni janga la kijamii linalohitaji hatua za haraka na za pamoja.

Akizungumza katika mdahalo huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Amon Mpanju alisema kuwa ili kutokomeza vitendo vya kikatili, ni lazima kujumuisha na malezi na kwamba mifumo lazima ianzie ngazi ya familia ambako kuna tamaduni zinazozunguka jamii.

Mpanju alisema eneo ambalo kunafanyika ukatili haliwezi kuwa na maendeleo kuanzia ngazi ya familia na kwamba ili kuondokana na hali hiyo, ni lazima kuwe na uwajibikaji kuanzia ngazi ya jamii kuhusiana na kile kinachofanywa na serikali katika kutokomeza ukatili.

Akifunga mdahalo huo kwa niaba ya Mwakilishi wa UN Women, mchambuzi wa shirika hilo, Godlizan Bakari alisema kazi ambayo Tanzania inafanya kukabiliana na ukatili wa jinsia ni kubwa na ni sehemu ya ajenda pana ya kikanda na kimataifa.

"Tunapokaribia kumbukumbu ya miaka 30 ya Azimio la Beijing, tuna fursa ya kipekee ya kuharakisha maendeleo ya kuondoa ukatili na kufanya maendeleo makubwa kuelekea usawa wa kijinsia yanaonekana.

"Mchakato mwingine unaoendelea ni maendeleo ya Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Kuondoa Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana (AU-CEVAWG) - mfumo wa kisheria wa kihistoria wa kuzuia na kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika bara lote," alisema.

Alisisitiza kwamba maono yao ya 2030 ni kuwa, katika ulimwengu ambao wanawake na wasichana wanaishi bila ukatili, jambo ambalo linawezekana endapo kutakuwa na ushirikiano.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA SONGEA**
**SHAURI LA MADAI YA NO.202409191000023404**
**ALLY SELEMAN MADAMBA———————MDAI**
**VERSUS**
**SONGEA MUNICIPAL ———MDAIWA NO .1**
**THE MTAA EXECUTIVE**
**OFFICER OF POLICE STREET ———MDAIWA NO.2**
**THE MTAA CAHAIRMAN OF POLICE STREET ———MDAIWA NO.3**
**CHRISTIAN MKUWA———MDAIWA NO.4**
**MWANAHAWA SAID ————MDAIWA NO.5**
**ERASTO LIMONGA ———MDAIWA NO.6**
**THE ATTORNEY GENERAL ———MDAIWA NO.7**

**KWA :**
**MWANAHAWA SAID**
**POPOTE PALE ULIPO**
**YAH.TAARIFA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA MADAI NO.202409191000023404 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA SONGEA UNAFAHAMISHWA KWAMBA**

Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu Tanzania kanda ya Songea saa tatu kamili asubuhi (3:00)siku ya tarehe 12/12/2024.

HIVYO BASI: Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyi iliyotajwa bila kukosa.

NAENDAPO :Hautafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kuumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo .

IMETOLEWA :kwa mkono wangu na mhuri wa Mahakama hii leo 20/11/2024.

————————————-
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA-SONGEA.**



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 26246/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late NICHOLAUS SABAI MAHEMBA of IPAGALA**
**Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**ESTER NICHORAUS SABAI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**
..................................................

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 12, 2024

....................................
**PETITIONER**
**Presented for filling this 8 day of 11,2024**
....................................
**RESIDENT MAGISTRATE**



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 290 LA 2023**
**LAURENCE NOEL NKOMOLLA**
**MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MOSES PETRO WAMBURA**
**MDAIWA/WADAIWA**
**WITO KUITWA SHAURINI**

**MOSES PETRO WAMBURA**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

LAURENCE N. NKOMOLLA Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala) Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 14/1/2025 saa 3;00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 Mwezi 11, 2024



**KUPOTEA KWA CHETI**



**LILIAN PHIDEL MWIDUNDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye **Index No. S0342/0030** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHAABAN ROBERT SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/KIN/271898/2024**



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 95/2024.**
**ONESMO HAULE—————— MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**HENEYATI KOMBA**
**COSMAS NCHIMBI}**
**MADIUS WELA}. ——— WAJIBU MAOMBI.**
**AGNESI MHAGAMA**
**KRISTOGUNUS HAULE**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

Agnesi Mhagama unataarifiwa kuwa Mleta Maombi amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 02/01/2025 saa mbili na nusu asubuhi kwaajili ya kutajwa.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri bila kujali uwepo wako .

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/12/2024.

————————————-
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**SONGEA**

## Kenya yatoa neno kuchelewa kuundwa Tume ya Uchaguzi

**NAIROBI,** Kenya

NAIBU Rais wa Kenya, Kithure Kindiki amesema ameona baadhi ya watu wakilaumu serikali juu ya kuchelewa kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) huku akisema serikali haina lawama.

Pia Kindiki jana alisisitiza pande zinazohusika katika mvutano wa kisheria kuhusu kuundwa upya kwa tume hiyo kufikia suluhu nje ya mahakama.

"Hii ni nchi inayoongozwa na sheria. Sheria ikiwepo, serikali haina uwezo wa kufanya chochote, kwa hivyo, tunaomba waliowasilisha kesi hizo waafikiane nje ya mahakama ili tuendelee na uundaji upya wa IEBC," alisema.

Hayo yalijiri baada ya kuibuka kwa mjadala kuhusu kuunda upya kwa IEBC, huku baadhi ya wananchi wakisema Rais William Ruto anafanya makusudi kutounda Tume hiyo.

Ilielezwa kuwa Kenya haijakuwa na wakala wa uchaguzi unaofanya kazi kikamilifu, miaka miwili tangu kuondoka kwa tume iliyopita. Na kwamba kukosekana kwa makamishna kunaifanya IEBC kushindwa kutekeleza majukumu yake muhimu, ikiwemo uwekaji wa mipaka na kusimamia uchaguzi mdogo.

Ilielezwa kuwa minong'ono hiyo pia ilichochewa na matamshi ya aliyekuwa makamu wa rais Rigathi Gachagua aliyesema ukosefu wa makamishna wa Tume ya Uchaguzi unatia doa katika uaminifu wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2027.

"Uchaguzi unaaminika kama mchakato muhimu. Ripoti ya Krigler ilipendekeza Tume ya Uchaguzi iwepo miaka mitatu kabla ya uchaguzi. Sasa tuna takriban miaka miwili na nusu bila IEBC na watu wanaweza kusoma ufisadi," alisema Gachagua.

Katika hafla tofauti, kiongozi wa Chama cha Wiper Kalonzo Musyoka pia aliwakashifu Rais William Ruto na Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetangula kwa kuchelewesh' uundaji wa IEBC.

"Nchi kama yetu inawezaje kujisimamia ikiwa hatuna Tume ya Uchaguzi? Uchaguzi Mkuu ni 2027, hii ni 2024, ni lini Tume hii itaundwa?," aliuliza.

Kalonzo alidai kuwa serikali, kupitia wawakilishi, ilihamia kortini kumzuia kiongozi wa chama cha Azimio Koki Muli aliyetaka kuwa sehemu ya jopo linalopaswa kuunda upya IEBC.

Kuna vikwazo vya kisheria ambavyo vimekuwa changamoto katika kutekelezwa kwa jopo la uteuzi wa IEBC. **TRT**



Rais wa Russia, Vladimir Putin na aliyekuwa Rais wa Syria, Bashar Al Assad aliyepinduliwa madarakani na waasi na kupatiwa hifadhi Russia. **PICHA: MTANDAO**

# Rais aliyepinduliwa Syria apewa hifadhi Russia

**MOSCOW,** Russia

IKULU ya Russia imesema aliyekuwa Rais wa Syria, Bashar al-Assad pamoja na familia yake wamepewa hifadhi Moscow kutokana na sababu za kibinadamu, baada ya waasi kuchukua udhibiti wa mji mkuu wa Damascus sambamba na kupindua utawala wake.

Wakati hayo yakijiri, jana Assad alitoa wito kwa waasi hao kwamba makabidhiano ya madaraka yafanyike kwa amani.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani Joe Biden alisema ni lazima Assad awajibishwe kwa vitendo vya mauaji na mateso kwa maelfu ya Wasyria. Na kwamba Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa jana lilifanya mkutano wa dharura na wa faragha ili kujadili hali inayoendelea Syria.

Aidha, waasi wa Syria walitoa marufuku ya watu kutembea nje usiku hadi saa 11 asubuhi. Tangazo lililojiri baada ya waasi hao kuchukua udhibiti wa mji mkuu wa Damascus na kuangusha utawala wa Rais Assad.

**Naibu Waziri Mkuu wa Uingereza, Angela Rayner, alisema kile kinachohitajika kwa sasa ni uthabiti wa kikanda akisema udikteta na ugaidi umesababisha madhila makubwa kwa watu wa Syria.**

Waasi hao pia walisema kwamba Rais Assad ameikimbia nchi na kwamba watakabidhi mamlaka kwa baraza la mpito. Huku raia wa Syria wakionekana kumiminika barabarani, wakishangilia baada ya waasi kusitisha utawala wa kiimla wa familia ya Assad wa miaka 50.

Ilielezwa kuwa wananchi hao walikusanyika mjini humo wakipeperusha bendera ya taifa hilo. Wengine walionekana wakiingia katika ikulu ya rais na maeneo mengine ya familia ya Assad baada ya rais na maofisa wengine wa serikali kuikimbia nchi.

Imeripotiwa pia kwamba watu waliingia katika ubalozi wa Iran mjini Damascus na kuharibu ofisi za ubalozi huo kando na kupora mali. Ikielezwa kuwa kuangushwa kwa utawala wa Assad ni pigo kwa Iran na washirika wake ambao wako katika mgogoro wa takriban mwaka mmoja na Israel.

Awali mshirika wa karibu wa Assad, Russia kupitia wizara yake ya kigeni ilisema rais wa Syria Assad aliondoka madarakani na kuitoroka nchi huku akitoa maagizo ya kukabidhi madaraka kufanyika kwa amani huku wizara hiyo ikisisitiza kuwa Russia haikuhusika na mazungumzo ya kuondoka kwake.

Ilielezwa kuwa Moscow ilikuwa na wasiwasi mkubwa juu ya matukio ya Syria na kuhimiza pande zote kujizuwia na vurugu na kusuluhisha masuala yote ya uongozi kupitia njia za kisiasa.

Hata hivyo, Russia ilisema inawasiliana na makundi yote ya upinzani Syria kuhakikisha hilo linafanyika. Ilielezwa kwamba Abu Mohammed al-Golani, kamanda wa zamani wa kundi la Qaida aliyekata mafungamano yake na kundi hilo miaka mingi iliyopita anaongoza kundi kubwa la waasi nchini Syria na anatarajiwa kuhusika kutoa muelekeo wa mustakabali wa taifa hilo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, alisema kwa sasa Syria haitakiwi kuanguka katika mikono ya makundi mengine yaliyo na itikadi kali. Akihimiza ulinzi kamili wa makundi ya kidini na makabila ya wachache kama ya Wakurdi na Wakristo.

Naibu Waziri Mkuu wa Uingereza, Angela Rayner, alisema kile kinachohitajika kwa sasa ni uthabiti wa kikanda akisema udikteta na ugaidi umesababisha madhila makubwa kwa watu wa Syria.

Mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa kwa Syria, Geir Pedersen pia alisema ukurasa mpya umefunguliwa nchini humo na anatumai utakuwa wa amani, maridhiano, uadilifu na unaowajumuisha Wasyria wote. **REUTERS /DW**

## HABARI MICHEZO

# TIMU ZA CHAMPIONSHIP NAZO ZAJIBU MAPIGO KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mfululizo wa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara kupata ushindi kwenye mechi za raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), maarufu Kombe la FA, zinazoshiriki Ligi Championship juzi nazo zilijibu mapigo.

**Jumla ya timu nne zilizo Championship, juzi zilipata ushindi kwenye michezo yao kati ya mechi saba zilizochezwa.**

Timu hizo ni Geita Gold, Mbeya Kwanza, Kiluvya FC, na Bigman, ambazo zimefanikiwa kuendelea na safari ya raundi ya nne, katika kampeni ya kusaka bingwa atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Geita Gold ikiwa Uwanja wa Nyankumbu, iliichapa Ruvu Shooting mabao 2-0, yote yakifungwa na Jackson Suluja, dakika ya 23 na 71, huku kwenye Uwanja wa Nangwanda Mtwara, Mbeya Kwanza ikipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mabao FC ya Shinyanga, mechi ikipigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara, Kiluvya FC ikapata ushindi mabao 4-0 dhidi ya African Lyon katika mchezo uliofanyika Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Nayo timu ya Bigman FC iliiondosha mashindanoni Soccer City kwa mikwaju ya penalti 3-2, baada ya sare ya bao 1-1 kwa dakika 90 za mchezo.

Timu pekee ya Championship ambayo ilitolewa juzi kwenye michuano hiyo ni Mbuni FC, iliyosukumizwa nje kwa mikwaju ya penalti 4-2 na Giraffe Academy, zikiwa zimetoka sare ya bao 1-1 dakika 90 za mchezo.

Timu mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara, Prisons na Kagera Sugar juzi zilifanikiwa kutinga raundi ya nne kwa kushinda michezo yao, Kagera Sugar ikishinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, dhidi ya Rhino Rangers, bao pekee la washindi likifungwa na Tariq Seif dakika ya 82, Wajelajela wao walipata ushindi wa mabao 4-2, Uwanja wa Sokoine Mbeya, mabao yote yakifungwa na Beno Ngassa dakika ya 46, 49, 59 na dakika za nyongeza kabla ya mechi kumalizika.

**AHSANTE...**



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko, akimkabidhi cheti cha udhamini, Meneja wa Mawasiliano wa Barrick, Georgia Mutagahywa, kutokana na kampuni hiyo kuwa moja wa wadhamini wa mbio za UDSM Marathon zilizofanyika mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, na wengine ni viongozi wa chuo hicho. **MPIGAPICHA WETU**

# *Magese akabidhi zawadi Samia Fashion Festival*

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAMITINDO wa Kimataifa Millen Happiness Magese amekabidhi zawadi ya Sh. milioni tatu kwa Mwanamitindo Elizabeth Masuka, aliyeibuka mshindi wa Shindano la Urembo la 'Samia Fashion Festival Zanzibar 2024'.

Magese aliyekuwa Jaji Mkuu wa shindano hilo, alikabidhi hundi ya fedha yenye thamani hiyo jijini Dar es Salaam ambapo alimwandalia chakula cha usiku mwanamitindo huyo na fedha hizo zikitolewa na Kampuni ya Millen PRIVE $ Co kupitia Millen PRIVE Lifestyle ambayo yeye ndio Mkurugenzi Mkuu.

Taarifa ya mwanamitindo huyo Mtanzania anayeishi nchini Marekani, aliyoitoa kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, ameeleza kuwa katika tamasha la Samia Fashion Festival Zanzibar yeye alikuwa Jaji Mkuu hivyo pamoja na kutangaza washindi wa tamasha hilo, aliona umuhimu wa kuitambua kazi kubwa iliyofanywa na wanamitindo walioshiriki usiku huo na kumtangaza Elizabeth Masuka kuwa mwanamitindo bora wa tamasha hilo.

"Tunafahamu kulikuwa na Samia Fashion Festival Zanzibar ambalo liliandaliwa na dada yangu Khadija Mwanamboka na katika tukio hilo nilikuwa Jaji Mkuu, hivyo baada ya kutangaza washindi, niliona umuhimu wa kuitambua kazi kubwa iliyofanywa na wanamitindo walioshiriki usiku huo na kumtangaza Elizabeth Masuka kuwa Mwanamitindo Bora wa Samia Fashion Festival Zanzibar mwaka 2024.

"Nimetoa fedha hizi kwanza kwa kutambua mchango wa wanamitindo wote ambao wamefanya kazi kubwa na nzuri wakati wa tamasha hilo, lakini fedha hizo ni katika kuwatia moyo wanamitindo wanaochipukia katika medani za Wanamitido na tatu nimetoa fedha kwa Elizabeth Masuka kwa kutambua yeye ndio Mwanamitindo bora wa Samia Fashion Festival Zanzibar mwaka 2024," alisema Magese.

Aidha, alisema amefurahishwa kufanyika kwa Samia Fashion Festival Zanzibar kwani limethibitisha nafasi na umuhimu wa wanamitindo nchini Tanzania, lakini pia kutoa nafasi ya vijana wa Kitanzania kuonesha uwezo wao katika kutawala Jukwaa la wanamitindo.

Kwa upande wa Elizabeth, alisema kukutana kwa mara ya kwanza na Millen ilikuwa ni ndoto iliyotimia na amefurahi kumuona ana kwa ana na kwa jinsi alivyo na mafanikio.

"Nimejifuza kitu kipya kutoka kwake, zawadi ambayo alinipa ilikuwa furaha yangu ya pili baada ya kazi nzuri ambayo imefanyika, namshuru sana na kumuombea Mungu aendelee kumweka kwa ajili yetu, ni mtu mwema sana, kutoka kwake niliona mtu ambaye anataka kuona wanamitindo wengine nchini Tanzania wakifanikiwa," alisema.

## Serengeti Boys yajiimarisha zaidi Uganda

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Soka ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), kinaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Afrika (AFCON U-17), zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Michuano ya CECAFA U-17 yanatarajiwa kufanyika kuanzia Jumamosi hadi Desemba 28, mwaka huu, jijini hapa.

Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo, alisema jana kikosi cha Serengeti Boys, kiliwasili mapema ili kujiweka katika mazingira chanya kuelekea michuano hiyo.

Mirambo alisema wamejipanga kuja kuwania taji hilo na wanaamini watafikia malengo kutokana na maandalizi mazuri waliyofanya.

"Timu iliwasili hapa (Kampala) jana (juzi), ikaanza mazoezi mepesi ya kuweka miili sawa na itaendelea na programu zake vema, ndio maana tumewahi kufika katika kituo cha mashindano," alisema Mirambo.

Aliongeza hakuna mashindano mepesi, lakini anaamini Serengeti Boys itaendelea kuwafurahisha Watanzania.

## TOC yaagiza kuunda Kamisheni za Michezo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya Olimpiki Tanzania (TOC), imeviagiza vyama na mashirikisho ya michezo nchini kuunda Kamisheni ya Mchezo wao ikiwamo kufuata maelekezo yao ili kuhakikisha taifa linapiga hatua katika sekta hiyo.

Hayo yalisemwa na Katibu wa TOC, Filbert Bayi, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa uchaguzi wa Kamisheni ya Wanamichezo TOC, uliofanyika jijini Dodoma na kuhudhuriwa na wawakilishi wa vyama husika.

Bayi alisema TOC inaamini katika vyama vya michezo na kwamba kukiwa na Kamisheni ya Wachezaji itasaidia kwa kiasi kikubwa kuibua vipaji vya chipukizi, lakini pia uwapo wa nidhamu kwa wachezaji wa mchezo husika.

Alisema wao kama TOC, wako tayari kufanya kazi na Kamisheni ya Wanamichezo hususan katika masuala muhimu ya kupeleka mapendekezo yao kimatiafa ili kuhakikisha wanashiriki katika michezo ya kimataifa, ikiwamo kutambulika kupitia vyama husika.

"Kamisheni ya wachezaji mna nafasi kubwa kuhakikisha michezo inasonga mbele kwa sababu mna uwezo wa kushauri viongozi wa vyama na mashirikisho kuhusu maendeleo ya michezo," alisema Bayi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VLAHOVIC AWANIWA EPL

ARSENAL, Chelsea na Manchester United bado wanavutiwa na Dusan Vlahovic, huku Juventus wakifikiria kumuuza mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 24, endapo kama atakubali mkataba mpya. ***(TBR Football)***

### SALAH MKATABA MPYA

LIVERPOOL imetoa ofa ya mkataba mpya kwa mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, 32. ***(Athletic)***

### DIJK NAYE KUFUNGWA

LIVERPOOL pia wanatazamia kuwafunga beki wa kati wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 33, na mlinzi wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold (22), kwa mikataba mipya. ***(Star)***

### ZUBIMENDI ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inaweza kuharakisha kuipiku Liverpool katika mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, kutoka Real Sociedad. ***(Football Insider)***

### WAKWAMA KWA CHERKI

JITIHADA ZA Crystal Palace kumsajili winga wa Lyon, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 21, zimezuiliwa na wababe wa Ulaya Paris St-Germain pamoja na Borussia Dortmund walioojiunga katika kinyang'anyiro hicho. ***(Sun)***

### YILDIZ AMULIKWA VILLA

KLABU ya Aston Villa ni moja kati ya klabu nne za Ligi Kuu England zinazomtaka winga wa Juventus na Uturuki, Kenan Yildiz mwenye umri wa miaka 19, ambaye klabu yake inaweza kumuuza kwa takriban pauni milioni 66. ***(BirminghamLive)***

### ATAKIWA AC MILAN

AC Milan ina nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea, Carney Chukwuemeka mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia anawavutia Celtic. ***(Soccer Italia)***

### ENDRICK HAONDOKI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid mwenye umri wa miaka 18, Endrick, ameamua kutoondoka kwa mkopo Januari na ataendelea kupigania naamba. ***(Marca)***

### KVARATSKHELIA KUSAINI

WINGA wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 23, anakaribia kusaini mkataba wa nyongeza na Napoli hadi 2029. ***(Corriere dello Spori)***

### ALLEGRI BASI TENA

KLABU ya West Ham ilimchukulia Massimiliano Allegri kama mrithi wa kocha wa sasa Julen Lopetegui, lakini mahitaji yake ni makubwa mno. ***(Football Insider)***

DOND KA
MAG YA




# MBAPPE: NINA NJAA SANA YA MAFANIKIO REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

KYLIAN Mbappe amejilaumu kwa mwanzo mgumu katika msimu wake wa kwanza katika Klabu ya Real Madrid kwa kusema "nina njaa kupita kiasi na sina subira" wakati wa mahojiano yake ya kwanza Jumapili, tangu ajiunge na klabu hiyo.

**Mbappe amefunga mabao 11 katika mechi 21 alizoichezea Madrid katika michuano yote kufikia sasa, likiwamo bao moja katika ushindi wao wa 3-0 wa LaLiga dhidi ya Girona Jumamosi, lakini amekabiliwa na ukosoaji wa kutokuwa kwenye kiwango cha juu.**

Katika mahojiano ya saa moja na Canal+ Clique - yaliyorekodiwa mapema wiki hii nyumbani kwake huko Madrid - Mbappe alijadili wakati wake katika timu yake mpya hadi sasa, na pia kutokuwapo kwake kwenye vikosi viwili vya mwisho vya Timu ya Taifa ya Ufaransa, na kuondoka kutoka Paris Saint-Germain.

"Real Madrid ni sehemu mpya, klabu na mazingira mapya," alisema Mbappe.

"Nitakuwa na mafanikio hapa. Mwanzoni nilikuwa na njaa sana, haikuwa nzuri kwangu, kwa sababu sikuwa na subira. Lakini nina shauku na nina ushindani. Wakati mwingine hiyo inaenda kinyume na mimi."

Mbappe alifunga katika mchezo wake wa kwanza kwa Madrid wa ushindi wao wa mabao 2-0 dhidi ya Atalanta kwenye UEFA Super Cup, na kufunga mabao sita zaidi Septemba.

Kisha akafunga mabao mawili katika michezo tisa - ikiwa ni pamoja na kufungwa na Lille, AC Milan na Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kichapo cha 4-0 kutoka kwa Barcelona - kabla ya kufunga dhidi ya Getafe na Girona mwezi huu.

"Haujakuwa mwanzo mzuri wa msimu huu, lakini tunajiandaa kwa mataji, ambayo ndiyo muhimu," alisema Mbappe.

"Mwanzo si vile tulivyotarajia, lakini kwa Madrid unapaswa kusubiri nusu ya pili ya msimu. Hapo ndipo unapohukumiwa."

Baada ya Euro 2024 ya kukatisha tamaa - ambapo alicheza akiwa amevunjika pua - nahodha Mbappe aliichezea Ufaransa katika mapumziko ya kimataifa ya Septemba.

Kisha alikosa michezo ya nchi yake Oktoba, baada ya kupona majeraha, na kuachwa na kocha Didier Deschamps kwa mechi mbili mwezi uliopita, na kusababisha uvumi juu ya mustakabali wake wa kimataifa.

"Timu ya Taifa ya Ufaransa daima imekuwa kiwango cha juu zaidi," alisema.

"Mapenzi yangu kwa Timu ya Taifa ya Ufaransa hayajabadilika, ndio nimeikosa kwa sababu sijakaa kwa muda mrefu, Septemba nilimwomba kocha asiniite, nilikuwa nimefika Madrid, nilikuwa na likizo fupi sana kocha alisisitiza niende.

"Mnamo Oktoba nilijeruhiwa. Sikuwa kwenye orodha. Kulikuwa na majadiliano, na kocha akaniambia ni bora asiniite Novemba. Yeye ndiye bosi, niko nyuma yake. Nilitaka niende, lakini siwezi kuhoji kwa nini hawakuniita."

Mbappe pia alizungumzia kuondoka kwake PSG, ambayo imesababisha vita vya kisheria kati ya mchezaji na klabu kuhusu madai ya kutolipwa mshahara na bonasi.

"PSG ilikuwa na maana kubwa kwangu. Nilikaa miaka saba pale, ni mahali pazuri sana, katika nyakati nzuri na mbaya. Nilikuwa na miaka saba isiyo ya kawaida.

"Nilikuwa na migogoro na watu, nilitetea haki yangu kama mchezaji, lakini hiyo haikuwakilisha klabu, sikuwahi kuchanganya hilo na wachezaji, watu wa akademi na kikosi.

"Mashabiki wanasema Kylian hajali, wanafikiri ilikuwa ni burudani kwangu, kabla ya kwenda Madrid. Bado natazama mechi za PSG, siku zote nimedumisha mahusiano na klabu. "

**Nitakuwa na mafanikio hapa, nina shauku na nina ushindani, wakati mwingine hiyo...**

# SIMEONE AKUNWA NA KIWANGO CHA GRIEZMANN




**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, alisifu matokeo ya wachezaji wake wa akiba baada ya timu yake kupata ushindi wa tisa mfululizo katika michuano yote kwa kuifunga Sevilla 4-3 kwenye La-Liga Jumapili.

Atletico walipata ushindi wa mabao 3-1 katika kipindi cha pili wakisaidiwa na waliotokea benchi, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa winga wa Brazil, Samuel Lino, ambaye alisawazisha kabla ya Antoine Griezmann kufunga mawili.

Huku Atletico Madrid wakiwa wameshika nafasi ya tatu kwa pointi 35, pointi moja nyuma ya Real Madrid na tatu tu nyuma ya vinara Barcelona, kocha huyo wa Argentina alitaja uchezaji wa wachezaji wa akiba kama ufunguo wa kuifanya timu yake kuwa kwenye mbio za kuwania taji.

"Timu inafanya kazi vizuri sana. Inanifurahisha wakati wale wanaosubiri wanaingia kwenye mechi vizuri. Kwa sababu hiyo ndiyo nguvu ya kusalia kwenye mchezo," alisema Simeone baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Wote wamecheza tangu tumeanza msimu na wamecheza sana, karibu wote. Wengine wametumia vema nafasi walizopewa, wengine wanajaribu kuimarika ili kupata zaidi.

"Bao la Lino linanifurahisha kwa sababu amekuwa akilitafuta. Leo (juzi) alifunga bao muhimu na litampa hali ya kujiamini anayohitaji.

"Leo (juzi) timu ilinifurahisha sana na majibu waliyopata kwa mabadiliko."

Nyota wa Atletico na mfungaji bora wa muda wote, Griezmann alifunga mabao mawili, na kupata sifa kutoka kwa kocha wake.

"Ni mtu ambaye ametoa kila kitu kwa Atletico Madrid."

# Nani atangaza rasmi kustaafu

**LISBON,** Ureno

WINGA wa zamani wa Ureno, Nani, ambaye alishinda mataji manne ya Ligi Kuu ya England na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Manchester United, ametangaza kustaafu kucheza soka la kulipwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alianza maisha yake ya soka katika Klabu ya Sporting CP kabla ya kusajiliwa na Kocha wa zamani wa Man United, Sir Alex Ferguson, mwaka 2007 na kisha kuondoka na kujiunga na Fenerbahçe kwa mkataba wa kudumu mwaka 2015.

Nani alichezea klabu 10 kwa jumla katika maisha yake ya miaka 19, akicheza nchini Uturuki, Hispania na Marekani.

Alisaini katika Klabu ya Estrela Amadora - timu kutoka kitongoji alichozaliwa mwanzoni mwa 2024.

"Kama kila mtu anavyojua, kila kitu kinafikia mwisho," alisema Nani katika taarifa.

"Nimechukua muda wa kufanya uamuzi muhimu sana. Labda uamuzi muhimu zaidi wa maisha yangu ya soka, ambayo ni uamuzi wa kuacha kucheza kama mchezaji wa kulipwa. Nitaweka viatu vyangu chini. Lakini ninafanya hivyo kwa hisia ya wajibu.

"Ninaamini ilikuwa kazi nzuri, kazi iliyojaa mafanikio mengi."

Nani alifunga mabao 130 katika zaidi ya mechi 620 za soka na alikuwa sehemu ya timu ya Ureno iliyofanikiwa kutwaa taji Euro 2016.




# Arteta: Arsenal ilistahili ushindi



**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema kwamba, Arsenal walistahili ushindi baada ya kutoka sare na Fulham Jumapili, lakini alikiri ubora uliooneshwa na wenyeji pale kwenye dimba la Craven Cottage ulikuwa ni wa hali ya juu.

Beki William Saliba aliokoa pointi kwa Arsenal dakika ya 52 baada ya Raul Jimenez kuwafungia Fulham katika kipindi cha kwanza.

"Tuna moyo kwamba hatukushinda. Tulistahili kabisa kushinda," alisema kocha Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Huo ndio ubora wa upinzani, kwa hiyo huwezi kulia juu yake."

"Tulitengeneza nafasi zote, lakini ni ngumu sana kushambulia."

Arsenal walimiliki mpira kwa asilimia 70 na bao la Bukayo Saka lilikataliwa kwa madai ya kwamba aliotea.

"Tulifanya karibu kila kitu tulichohitaji kufanya ili kushinda, lakini wapinzani wetu nao walikuwa bora sana.

"Haitoshi kama hutafunga tatu, nne au tano. Ikiwa pande pinzani zitacheza mipira 11 ya moja kwa moja nataka kushinda 11. Tunataka kushinda kwa asilimia 100," alisema.

Fulham wamekuwa mwiba kwa Arsenal, kwa kufanikiwa kupata ushindi wao msimu uliopita kwa kushinda nyumbani na kutoka sare kule Emirates.

Sare hiyo ilimaanisha Arsenal kusalia nafasi ya tatu kwenye msimamo, pointi mbili nyuma ya Chelsea na sita nyuma ya vinara wa ligi Liverpool.

## HABARI MICHEZO

# FADLU AANIKA SABABU

INATOKA UKURASA 24

michezo hii ya Afrika ni kwamba kila mmoja lazima ashinde nyumbani kwake, kushinda ugenini inakuwa kama ni bonasi kama siku hiyo utakuwa upo vizuri," alisema.

# Nyuma ya pazia Simbu...

INATOKA UKURASA 24

sha, sasa mimi uasi wangu unatoka wapi kama si chuki binafsi hizi, na kama walikuwa wameniengua kwa nini hawakunipa taarifa hadi wasubiri kunidhalilisha ukumbini," alihoji Simbu kwa masikitiko na kuongeza.

"Mzee Tandau ndiye alikuwa mkuu wa msafara na Julai 25 alikaririwa na vyombo vya habari akiwa Paris, kwamba taratibu zote zimeishakamilika ikiwamo usajili wa mavazi watakayotumia, sasa mbona wasimamizi wa Paris Olimpiki walipitisha tutumie Xtep, kosa langu ni lipi?," Alihoji.

Kitendo hicho cha uongozi wa TOC, kimelaaniwa na wadau wengi wa michezo, ukiwamo wa Shirikisho la Riadha Tanzania, na kwamba si cha kufumbiwa macho na kuachwa kipite hivi hivi.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Katibu Mkuu wa RT, Wakili Jackson Ndaweka, alisema kumuengua Simbu kwenye uchaguzi huo ni jambo moja, lakini kumdhalilisha ni jambo la kusikitisha sana.

"Mchezaji mwenye hadhi ya Alphonce Simbu, anapodhalilishwa na watu kiasi cha kusahau kwamba kipaumbele cha michezo yoyote huwa ni wachezaji ni suala ambalo halipaswi kuchukuliwa kirahisi. Hata Imani ya Olimpiki (Olympic Movement), inasema wachezaji ndio kipaumbele," alisema Wakili Ndaweka na kuongeza.

"Kwa miaka ya hivi karibuni kuanzia 2016 kwa mara ya kwanza Simbu aliposhiriki Michezo ya Olimpiki, ndiye mchezaji aliyefanikiwa zaidi katika michezo inayoratibiwa na Kamati ya Olimpiki Tanzania na ile ya mashirikisho, kuliko mchezaji mwingine yeyote yule wa Tanzania si tu riadha, bali michezo yote."

Alifafanua kuwa, Simbu alishika nafasi ya nne wakati wa Rio Olimpiki nchini Brazil, nafasi ya tatu na kupata medali ya Shaba wakati wa mashindano ya Dunia London 2017, nafasi ya tano Tokyo Olimpiki na nafasi ya pili na kushinda medali ya Fedha Michezo ya Jumuiya ya Madola Birmingham Common 2022.

"Hakuna mchezaji mwingine amekuwa na rekodi nzuri ya uwakilishi wa nchi zaidi ya Simbu katika kizazi cha sasa. Hii ni mbali na mashindano mbalimbali ya kimataifa ambayo ameipeperusha bendera ya nchi ikiwamo London Marathon, Mashindano ya Dunia ya Majeshi 2023, Mashindano ya Afrika ya Majeshi 2024 alipotwaa Dhahabu na Valencia Marathon ya 2024 nafasi ya nne, hivyo hakupaswa kufanyiwa hivi, kwani hii inaleta picha mbaya na kuwavunja moyo wachezaji," alisisitiza Ndaweka.

Wakili Ndaweka, alisema Kiongozi yeyote anayejiona ana haki ya kumdhalilisha shujaa huyu wa nchi hawatamfumbia macho.

Baadhi ya wajumbe wa mkutano wa KAWATA ambao waliomba kuhifadhiwa majina yao, walisema TOC haikumtendea haki Simbu na itawavunja moyo wachezaji kuipambania nchi, kwani mchango wao unaonekana hauthaminiki.

Walieleza kuwa, Simbu hapaswi kukandamizwa kwa suala hilo la vifaa, kwani lilikuwa ni baina ya TOC na RT, wachezaji hawahusika kwa kuwa hupokea maelekezo kutoka kwa viongozi.

Itakumbukwa, kuelekea Olimpiki Paris, kuliibuka mvutano wa matumizi ya vifaa kwa wanariadha kati ya TOC na RT, lakini mwisho wa siku vifaa vilivyotumika Paris vilikuwa ni vile vilivyotolewa na shirikisho hilo la Riadha.

Aidha, wadau wengine wanadai kuwa vita ya Uchaguzi Mkuu TOC nayo imechangia hilo kwani Simbu alianza kung'ara wakati rais wa RT alikuwa Anthony Mtaka ambaye aliweka nia ya kugombea nafasi ya urais katika uchaguzi huo uliofutwa hivi karibuni ambapo alikuwa akichuana na Tandau.

# YOSSO WA TANZANIA KAZINI MASHINDANO YA CAF U-15

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

TIMU ya Taifa ya Soka ya vijana ya wavulana umri chini ya miaka 15, inatarajia kukutana na Burundi katika mechi ya ufunguzi ya michuano ya Shule ya Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa St. Mary's ulioko jijini hapa.

**Mashindano hayo ni maalumu kwa ajili ya kusaka tiketi ya kuuwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), katika michuano ya Afrika (CAF U-15), itakayofanyika baadaye mwakani.**

Mechi hiyo ya yosso wa Tanzania na Burundi itachezwa kuanzia saa 3:00 asubuhi nabaadaye saa 10:00 jioni kikosi hicho kitashuka kucheza dhidi ya Somalia.

Mkurugenzi wa Mashindano wa CECAFA, Mosi Yusuph, ameliambia gazeti hili maandalizi ya michuano hiyo yamekamilika.

Mosi alisema baada ya kukamilisha taratibu za vipimo, timu zilizobakia katika mashindano kwa upande wa wavulana ni tano huku nchi nne zikichuana kwa upande wa wasichana.

"Tunashukuru kuona mashindano haya yanafanyika tena katika ukanda wetu, ni daraja muhimu katika kuwaandaa wachezaji wetu, kila kitu kitafanyika kwa mujibu wa taratibu," alisema Mosi.

Aliongeza kuwa, kutokana na timu kuwa chache, mashindano hayo sasa yatachezwa kwa mfumo wa ligi na nchi itakayovuna pointi nyingi itatangazwa kuwa mabingwa.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa, Tanzania itashuka tena dimbani kucheza na wenyeji Uganda kesho asubuhi na keshokutwa itamalizia kwa kuwavaa Rwanda.

Wakati huo huo, Timu ya Wasichana ya Tanzania itaanza kampeni ya kuwania taji hilo leo kwa kucheza dhidi ya Rwanda na kesho itakutana na Uganda.

Yosso hao wasichana watamaliza michuano hiyo keshokutwa kwa kupambana na wenzao kutoka Burundi.




Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Anga Tanzania (TCAA), wakishiriki mbio za UDSM Marathon zilizoandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kufanyika mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *TCAA washiriki UDSM Marathon wakiadhimisha siku yao duniani*

**Na Moshi Lusonzo**

WAFANYAKAZI wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), wameendelea kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga Duniani (ICAD), kwa kushiriki katika mbio za Marathon zilizoandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Mbio hizo zilizoongozwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, zilihudhuriwa pia na Mkuu wa chuo hicho, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete .

Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga Duniani ambayo kilele chake kilifanyika Desemba 7, mwaka huu, yanaambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo michezo.

Kwa maadhimisho ya mwaka huu yanatimiza miaka 80 tangu kuanzishwa kwa siku hiyo, mwaka 1944.

Watumishi wa TCAA licha ya kufanya kazi zao za udhibiti na kuongoza ndege, pia hushiriki katika michezo mbalimbali ikiwa ni hatua ya kujenga afya katika hali bora wakati wote.

# Michezo

Jumanne Desemba 10, 2024

Nipashe



## Mbappe: Nina njaa ya mafanikio Real

UKURASA 21

TAMBUKA...



Mshambuliaji wa Simba, Christian Leonel Ateba, akimtambuka beki wa CS Constantine ya Algeria kwenye mechi ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Mohamed Hamlaoi juzi nchini humo na wenyeji kushinda mabao 2-1. **PICHA: SIMBA**

## Nyuma ya pazia Simbu kuenguliwa Uchaguzi TOC

**Na Mwandishi Wetu**

KILICHOMKUTA mgombea wa nafasi ya Uenyekiti Kamisheni ya Wachezaji (KAWATA), ya Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Mwanariadha mahiri, Alphonce Simbu, katika uchaguzi uliofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki, kimedaiwa kuwa ni chuki na visasi.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Msimamizi wa uchaguzi huo, Henry Tandau, ambaye ni Makamu wa Rais TOC, alimwengua Simbu ukumbini mbele ya wapigakura, huku akimtuhumu kwamba ni muasi, alichochea wachezaji kutokuvaa vifaa vya Kampuni ya Asics vilivyokuwa vimeandaliwa na kamati hiyo, wakati wa Michezo ya Olimpiki Paris iliyofanyika Julai 26-Agosti 11, mwaka huu, badala yake wakatumia vya Xtep, ambao ni wadhamini wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT).

Licha ya mchakato wa usaili kufanyika, Simbu hakupewa taarifa kwamba ameenguliwa, hivyo kufika hadi mbele ya wajumbe akiamini anaenda kuomba kura, lakini Tandau hakutaja jina lake.

Simbu alipohoji, ndipo Tandau alipofunguka kuwa ni msaliti, hafai kuwa kiongozi kwa kuwa alishiriki kugomesha wanariadha kuvaa vifaa vya Asics badala yake wakatumia Xtep wakati wa Olimpiki Paris, hatua iliyoibua taharuki ya majibizano ya maneno ukumbini hapo.

Akizungumzia tukio hilo, Simbu alieleza kusikitishwa na kitendo hicho kisicho cha kiuanamichezo na kisichofuata taratibu, kwani mbali ya kumyima haki yake ya msingi, kimemdhalilisha mbele ya wapigakura na jamii kwa ujumla.

"Mimi nilitumia haki yangu kikatiba, nikachukua fomu na kujaza na kuirejesha ndani ya taratibu na hadi kufika kwenye usaili, ambapo suala hilo walinihoji na nikalitolea ufafanuzi kwamba mimi sina uwezo wa kuamua wachezaji wavae mavazi gani... kwani wanaosajili mavazi ya timu ni viongozi na hadi sisi tunaingia mashindanoni tulikuta vifaa vilivyosajiliwa ni vya Xtep na wasimamizi wa mashindano ndio walivyovipiti-

INAENDELEA UKURASA 23

# FADLU AANIKA SABABU KIPIGO SIMBA ALGERIA

**Na Adam Fungamwango**

### Asema walipaswa kushinda, awataja mabeki huku akitaka akili sasa kugeuziwa kwa Watunisia...

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amefunguka kuwa kichosababisha timu yake kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya CS Constantine ya Algeria ni makosa madogo kwenye eneo la ulinzi, pamoja na wachezaji kutofuata maelekezo yake aliyowapa watakapoingia kipindi cha pili.

Simba ilipoteza mechi hiyo ya raundi ya pili, Kombe la Shirikisho hatua ya makundi iliyochezwa, Uwanja wa Mohamed Hamlaoi jijini Constantine kwa mabao ya kujifunga ya Abdulrazack Hamza dakika ya 46 na Brahim Dib dakika ya 50, ambapo kabla ilipata bao la kuongoza dakika ya 24, lililowekwa wavuni na Mohamed Hussein 'Tshabalala.'

**Fadlu alisema katika mechi ya juzi ilipaswa kumalizika kwa Simba kushinda au pengine sare kama walinzi wake wasingefanya makosa na kutofuata maelekezo dakika za mwanzo za kipindi cha pili.**

"Mechi ilikuwa nzuri, ilipaswa kuisha kwa ushindi au pengine sare, tumepoteza mchezo kwa makosa madogo ya eneo la ulinzi, magoli yote ya wapinzani yalikuwa mepesi ya yanayozuilika, naamini wachezaji wangu wataendelea kujifunza na nina imani wataimarika," alisema kocha huyo.

Alisema katika dakika zote 90, wapinzani wao hawakutengeneza hatari yoyote kwenye lango lao, badala yake walikuwa wanategemea mipira iliyokufa na kona tu.

"Costantine hawajatengeza nafasi yoyote ya hatari dhidi yetu, tuliimiliki mechi kwa kiasi kikubwa, wao walikuwa wazuri kwenye mipira iliyokufa na niliwaambia wachezaji wangu kwenye dakika tano za mwanzo kipindi cha pili hatupaswi kuruhusu kona wala faulo, lakini hawakufanya hivyo na ndicho kilichotokea," alisema.

Kipigo hicho kinaifanya Simba kushika ya tatu kwenye msimamo wa Kundi A, CS Constantine ikiongoza ikiwa na pointi sita, Bravo do Maquis ya Angola, baada juzi kuifunga CS Sfaxien ya Tunisia mabao 3-2 inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi tatu kama Simba, lakini iko juu kwa kufunga mabao matatu, huku Watunisia wakiburuza mkia wakiwa hawana pointi.

Simba itashuka tena dimbani Jumapili ijayo, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kuwakaribisha waburuza mkia wa kundi hilo, CS Sfaxien.

Meneja Habari na Mawasiliano, Simba, Ahmed Ally, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kusahau matokeo ya juzi, badala yake kujiandaa kuujaza uwanja kwa ajili ya kusaka ushindi wa pili nyumbani, baada ya ule wa kwanza wa bao 1-0 dhidi ya Bravo do Maquis.

"Matokeo si mazuri, lakini haina athari yoyote katika kampeni yetu ya kuvuka hatua ya makundi, msingi katika

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >